Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 74 No. 175 | SHA'BAAN 1434 AH | JUNI 2013 | IHSAN 1392 HS | BEI TSH. 500/=

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Je! mnafanya kuwanywesha mahaji na kuustawisha Msikiti Mtukufu ni sawa na (kazi ya) yule anayemwamini Mwenyezi Mungu na Siku ya mwisho na akajitahidi katika njia ya Mwenyezi Mungu? Hawawi sawa mbele ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu Hawaongozi watu wadhalimu. (Taubah - 9:19)

Bunge la Uingereza lawa mwenyeji wa tukio la Kihistoria:

Lafanya sherehe ya kuadhimisha Karne moja ya Ahmadiyya UK

Na Jamil Mwanga, Dar es Salaam

Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) ametembelea Westminster (eneo ambalo ndipo zilipo ofisi kuu za Bunge la Uingereza pamoja na ofisi zingine za serikali) na kutoa hotuba katika hafla maaluum iliyoandaliwa na **Mhe. Ed Davey (MB)**ambaye pia ni (Katibu wa Nchi anayeshughulikia Nishati na Mabadiliko ya Hali ya Hewa) na viongozi wengine katika maadhimisho ya karne moja ya Jumuiya ya Waislam Ahmadiyya, Uingereza.

Kabla ya kuanza kwa ratiba rasmi, Khalifa Mtukufu, Hazrat Mirza Masroor Ahmad (a.t.b.a) alifanya mazungumzo ya faragha na Naibu Waziri Mkuu, Mhe. Nick Clegg (MB), Katibu wa Nchi anayeshughulikia Idara ya Mambo ya Ndani Mhe. Theresa May (MB), Katibu wa Nishati Mhe. Ed Davey (MB), Katibu Kivuli wa Mambo ya Nje Mhe. Douglas Alexander (MB), Mhe. Keith Vaz (MB) na Siobhain McDonagh (MB).

Ratiba rasmi ilianza saa saba na dakika tano mchana kwa hotuba fupi ya utangulizi iliyotolewa na Ed Davey, Katibu wa Nchi anayeshughulikia Nishati na Mabadiliko ya Hali ya Hewa. Hotuba hii ilifuatiwa na hotuba fupi zilizotolewa na Naibu Waziri Mkuu, Nick Clegg, Douglas Alexander, Katibu Kivuli wa Mambo ya Nje; na Theresa May, Katibu wa Mambo ya Ndani.



Kiongozi wa Jumuiya ya Waislam Ahmadiyya, Khalifa wa Tano, Hazrat Mirza Masroor Ahmad (a.t.b.a) akikaribishwa katika jengo/kumbi za Bunge na Naibu Waziri Mkuu pamoja na viongozi wengine wa Serikali pamoja na Bunge mnamo tarehe 11 Juni, 2013 huko Westminster, England.

Mhe. Ed Davey, Katibu wa Nchi anayeshughulikia Nishati na Mabadiliko ya Hali ya Hewa alisema:

"Kwa kweli ni jambo la heshima kwetu kuwakaribisha Jumuiya ya Waislam Ahmadiyya leo hii. Tunatambua fika jitihada za dhati zinazofanywa na Mtukufu (Hazrat Mirza Masroor Ahmad) katika suala zima la amani na pia kwa wanajumuiya Ahmadiyya. Hivyo, ni sahihi kabisa kwamba Wabunge wengi wako hapa kwa lengo la kuwashukuru kwa kuwa watu waaminifu na mfanyao juhudi katika jamii."

Mhe. Nick Clegg, Naibu Waziri Mkuu alisema:

"Jambo muhimu sana na jema ambalo Jumuiya ya Ahmadiyya imekuwa ikiendelea kuwafahamisha mamilioni

Endelea uk. 3

Kisa cha Nabii Issa (a.s.) Kusema Uchangani

Kutoka toleo lililopita

Na Mwl. Abdullah H. Mbanga - Dar es Salaam

Ukweli ni kwamba Nabii Isa (as) hakukiri shitaka hilo na kwa hiyo Makuhani walilazimika kutafuta mashahidi wa uongo dhidi yake, jambo ambalo hata hivyo hawakulifanikisha (tazama Marko 14:55, Mathayo 26:59). Hata walipojaribu kumshawishi kipofu mmoja aliyeponywa na Nabii Isa (as) iii awe shahidi wao dhidi ya Nabii Isa (as) ya kwamba alidai Ufalme, kipofu Yule alidai kuwa anamtambua Yesu kama Nabii tu. (Yoh.9:17).

Ndipo baada ya Baraza hilo kukosa shahidi wa kuwa auni, wakahamanika na wakaanza kuhaha kuwatafuta wanafunzi wa Nabii Isa (as) ambao hata hivyo hawakuwapo barazani. Wote walijificha kuhofu usalama wao, isipokuwa Petro ambaye alijipiga moyo konde na kufuatilia kesi hiyo akiwa amejibanza kwa mbali. Wakimkiabili Petro kwa maswali kupitia watu watatu tofauti. Lakini Petro siyo tu alikana kutoa ushahidi, bali pia alikana hata kumjua Nabii Isa (as) (Luka 22:57-60). Mchakato huu ulifanyika mbele ya Nabii Isa (as) ambaye ni mtuhumiwa. Ndiyo maana Petro alipomkana Nabii wake, Isa (as) alimtazama ndipo Petro akatoka nje na kulia sana (Luka 22:61-63). Hii ni kwa sababu aligundua kuwa siyo tu alikuwa amevunja ahadi aliyoitoa mwenyewe ya kuwa pamoja na Bwana wake katika mapambano, lakini pia alikuwa ameangukia katika kutimiliza bishara iliyotolewa na Nabii wa Mungu juu yake. Alibashiriwa kwamba angemkana Nabii Isa mara tatu kabla ya jogoo kuwika (Mathayo 26:34). Tukio hili la Petro kumkana Yesu (Nabii Isa as) limewafanya wasomaji wengi wa Injili kumhesabu Petro kuwa miongoni mwa wanafiki, kwa kuwa eti alidiriki kuikana imani yake hadharani kwa kuhofu usalama wake mbele ya Makuhani.

Lakini ilikuwa kweli Petro ni mnafiki basi bila shaka Nabii Isa (as) alikuwa ni Nabii mwenye bahati mbaya kuliko wote. Sifa za Petro ambazo

Endelea uk. 5

Tafsiri ya kwanza ya Qur'an Tukufu kwa Kiyao yaona jua

Na Alli Saidi Mosse

Siku moja mnamo Januari 1998, nikiwa nimeketi pamoja na wanajamaat wenzangu barazani mwa Masjid Salaam, niliitwa ofisini kwa Amir na Mbashir Mkuu wa wakati huo Maulana Sheikh Tahir Mahmud Khan, ambaye alinifahamisha kuwa Khalifa Mtukufu wa Nne Hadhrat Mirza Tahir Ahmad, aliagiza kuwa Qur'an Tukufu itafsiriwe kwa lugha ya Kiyao na kwamba mimi nimeteuliwa nifanye kazi hiyo. Taarifa hii nzito ilikuja baada ya takriban miaka kumi tangu kwa msaada wa Mwenyezi Mungu nilipokamilisha kazi ya kutafsiri vitabu vitatu kwa lugha ya kiyao, nikisaidiwa na wazee wawili wanajumuiya (sasa ni marehemu), Sheikh Issa Haarun na mzee Karuma Issaa mbao walikuwa wayao. Vitabu hivyo ni '***Baadhi ya aya zilizochaguliwa kutoka katika Qur'an Tukufu***', '***Baadhi ya semi za Mtukufu Mtume saw***' na '***Baadhi ya semi za Masih Aliyeahidiwa a.s***. Vitabu hivyo vilichapishwa na kusambazwa kama sehemu ya kusherehekea miaka mia moja tangu Jumuiya ya Waislam Waahmadiya ianzishwe (1889-1989) na Masih Aliyeahidiwa (as) Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad as.

Kwa vile ugumu wa kazi ya kutafsiri nilikwisha ufahamu, sikusita kumwambia Amir na Mbashir Mkuu kwamba

Endelea uk. 4

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

NENO LA ALLAH

Wakati Historia iliyotukuka ya Jumuiyya ya Waislam Waahmadiyya katika Afrika Mashariki inakamilika kuandikwa, hapana shaka yoyote kurasa zinazohusu harakati za kutafsiri Qur'an Tukufu katika Kiswahili, Luganda, Kikamba, Kiluwo na Kiyao zitaandikwa katika wino wa dhahabu. Kutanguliza dini mbele ya dunia, utumiaji wa akili kwa uangalifu, kujitolea kwa hali ya juu, kufanya utafiti ni sifa ambazo Mwenyezi Mungu Aliwapatia waliofanya kazi hii tukufu ya kuwafikishia waja wa Allah neno Lake katika Lugha zao.

Sheikh Mubarak Ahmad kwa pashau na shauku alijikita katika kutafsiri Qur'an Tukufu katika lugha ya Kiswahili. Upepo wa wakati huo ulikuwa unavuma kupinga wazo hilo la kutafsiri Qur'an Tukufu katika Lugha yoyote, walisema wengi hiyo haiwi wala haitakuwa. Hakukata tamaa, aliendelea kubukua na huku akiendeleza maombi. Mwaka 1953 ikatoka tafsiri safi ya Qur'an Tukufu yenye Kiswahili mwanana na yule simba wa uswahilini Sheikh Shaabani Robert alionesha furaha yake kwa kusema; "Ama kweli tafsiri hii ni mama wa Kiswahili".

Zakaria Kizito ambaye alikuwa mwanafunzi wa Sheikh Mubarak Ahmad huko Tabora akasadifu methali ya Kiswahili isemayo; "Ukikaa karibu na waridi hukosi kunukia". Aliporejea Kampala akawatangazia ndugu zake wote kwamba alikuwa na kazi moja tu nayo ni kutafsiri Qur'an Tukufu katika Lugha ya Luganda. Asubuhi na jioni alijifungia ndani kuifanya kazi hiyo na alifikiwa na mitihani mingi, lakini hatimaye mashua ikatia nanga pwani huku ikiwa imebeba tafsiri safi ya Qur'an Tukufu katika Luganda. Baganda wote wakaamsha mikono kumshukuru Mwenyezi Mungu na kumwambia 'Webale' - Akhsante.

Kenya nao hawakuwa nyuma katika harakati za kutafsiri Qur'an Tukufu. Kwa hivi sasa tunayo Qur'an Tukufu katika Lugha ya Kikamba, Kijaluo na Kikuyu.

Furaha yetu imezidi hapa Tanzania kutokana na kupokea tarehe 26/06/2013 Qur'an Tukufu katika Lugha ya Kiyao. Miaka michache iliyopita Bwana Alli Saidi Mosse ambaye amepata kuwa Katibu wa Taifa wa Tabligh na Amir Jamaat Tanzania aliwahi kutafsiri '*Baadhi ya Aya za Qur'an Tukufu katika Kiyao; Baadhi ya Hadithi za Mtukufu Mtume s.a.w.* na *Baadhi ya maandiko ya Masihi Aliyeahidiwa* katika Lugha hiyohiyo. Umahiri huo ulionesha dhahiri kwamba kazi hiyo anaiweza. Khalifa Mtukufu wa Nne rh, alimteua atafsiri Qur'an Tukufu kwa Kiyao. Kazi hiyo aliendelea nayo, bali ilikuwa inasuwasuwa mno kwa sababu kwa wakati huo alikuwa ameajiriwa Serikalini. Mara kwa mara alikuwa anapata barua kutoka Markaz za kutaka kujua maendeleo ya tafsiri hiyo katika Kiyao.
Bwana Alli Saidi Mosse alifika mahala na kufanya uamuzi. Na huo hasa ndio uamuzi wa busara. Aliacha kazi ili afanye kazi hii aliyotumwa na Khalifa wa Mwenyezi Mungu. Alhamdulillah, kazi hiyo sasa imekutana na alfajiri ing'arishayo nyoyo zetu. Hapana shaka malipo yote yako kwa Mwenyezi Mungu, lakini nasi tunayo sehemu ya kushukuru, kwani Waswahili husema 'Mcheza Kwao hutunzwa'.

Ni matumaini yetu makubwa kwamba Tafsiri hii ya Qur'an Tukufu katika Kiyao itawafikia ndugu zetu waliopo hapa Tanzania, Malawi, Zambia na Msumbiji ili hatimaye wakiuke kuta hizi na waweze kuingia katika nyumba ya Masihi Aliyeahidiwa - Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as).

MAONI: SAKATA LA KUCHINJA WANYAMA

Mhariri
Mapenzi ya Mungu

Naungana na Mwalimu Kais Ally wa Mkongotema Jamaat Madaba kwenye maoni yake yaliyochapishwa katika gazeti hili yenye kichwa cha hapo juu ya Mwezi Machi 2013.
Nilichotaka kuandika hapa amemaliza mwenyewe siyo vema jambo ambalo limekwishaelezwa lirudiwe. Nakubali kwa namna moja au nyingine kuwa ni kweli kuwa fujo za kidini na mauwaji chanzo kikubwa ni viongozi wenyewe wa dini. Nanukuu maelezo aliyotoa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza kuwa "Wachinjaji halali ni Waislamu", Pia Waziri Mkuu akasema hivyo hivyo baadaye akatumia lugha takatifu kuwa "Utaratibu ubakie kama ule wa kwanza". Mbona maana ni ile ile? Hapo mwanzo alikuwa anachinja nani? (Waislam) Viongozi wa dini wanazijua dini zote vizuri zaidi na sheria zake kuliko sisi ndiyo maana wanatufundisha sisi.
Naamini kuwa dini ni njia ya kwenda kwa Mungu, Uende kwa mguu, kwa baiskeli, pikipiki, gari, ndege n.k Lakini wote tunatakiwa tufike mahala hapo yaani kwa Mungu. Lakini njia hizo zina masharti yake. Kwa mfano anayesafiri kwa mguu ni lazima abebe posho ya kula njiani, na yule wa kusafiri na ndege ataamuliwa avae suti, hizo ndizo taratibu za kila njia (Kwa Waislam kama hizo za kuchinja mnyama).
Pia hapa duniani hakuna dini kubwa zaidi au ndogo zaidi, dini ni dini tu. Wote tunajua dini zote zinafundisha maadili mema kwa ajili ya jamii.
Sasa napenda niwaulize viongozi wa dini (Maaskofu wa Mwanza) Je, ni Msahafu gani au kitabu gani imeandikwa kuwa Mkristo akila nyama iliyochinjwa na Mwislam anatenda dhambi? Mwislam anakataa kula nyama isiyochinjwa na Mkristo kwa sababu sheria ya dini yake inamkataza. Kuna mambo mengi sana yanafanywa na Waislam kama masharti ya dini yao lakini sisi Wakristo tumeyaiga kwa vile ni mambo mema, mengine ni kwa manufaa ya jamii. Kwa mfano enzi zangu za miaka ya 1960 Wakristo waliamini kuwa kutahiri ni Uislamu. Lakini sasa limekuwa ni jambo la kawaida kwa wote baada ya kufumbuka kuwa kutahiri siyo Uislamu bali ni usafi, ingawa kwa Uislamu ni moja ya sheria ya dini. Yapo mambo mengi siwezi kueleza yote ambayo sisi Wakristo tunayafanya.
Mwislam mwanamume anapokwenda Msikitini kuswali anavaa kanzu na kofia, maarufu kwa kuitwa balksheh, nguo hizo huwa safi sana, na pia mwanamke huvaa nguo kwa kweli zinaashiria nia yake ya kwenda kusali, ni ndefu pia hufunika kichwa chake kwa kanga au nguo iitwayo baibui. Kwa sasa Wakristo wamegeuza kofia hizo ni fasheni asilimia 70 ya Wakristo huvaa kofia hizo, Maaskofu hao wa Mwanza walisahau hayo wameng'ang'ania la kuchinja tu.
Ukichunguza kwa undani zaidi utagundua kuwa Waislamu kuwa kweli wanatimiza maagizo ya Mwenyezi Mungu kutokana na matendo yao hapa duniani ya kusaidia sana jamii. Mfano Hapa kijijini petu wameingia Waislamu (Hamadia) wamejenga Msikiti wa kisasa ambao umeongeza kupendeza kwa kijiji chetu (ingawa wao siyo wengi) kuna muda serikali ya kijiji au viongozi wa kijiji wanaomba Mwalimu atangaze matangazo ya kijiji kwa kutumia spika (vipaza sauti) zao za kisasa ambazo husikika kijiji chote hata kijiji cha jirani pia cha Magingo. Hapa kijijini pana tatizo la muda mrefu la maji ya bomba, lakini Waislamu hao (Waahmadia) wamejitolea kuchangia maji hayo kiasi cha Shilingi Milioni saba, lakini kwa Wakristo hawajachangia hata mia mbovu. Maji hayo yakifika yatasambazwa kwanza kwenye Taasisi muhimu, kama Msikitini, Kanisani, Shuleni, Zahanati n.k. Kwa matumizi ya Taasisi hizo.
Kama Maaskofu hao watasema tusitumie maji hayo, kwa vile yamechangiwa na Waislam, kwa kweli Waumini wao watawageuka kwani taabu wanayopata sasa ya kufuata maji visimani, na sasa wamepata ukombozi hapo tutapingana nao.
Ishitoshe kuna shule za Sekondari za Kiislamu ina maana watoto wetu wa Kikristo wasisome kwa maana kuwa kama watakwenda kusoma huko watakuwa wameuegemea Uislamu? Hayo ni mawazo potofu pia ni kucheleweshe maendeleo ya nchi.
Nimesema kuna mambo mengi ya kidini yanafanywa na hao Waislam kwa manufaa hata ya sisi Wakristo ambao Maaskofu hao wameshindwa kuyataja ila uchinjaji tu! Hapo mnapotosha taifa. Kwa sasa macho yetu yapo kwenu ninyi viongozi wa dini tumeshatambua nani aleta vurugu hizi na mwishowe zitaingia hata kwa mtu mmoja mmoja. Mfano siku hizi kuna ndoa za mseto, Mwislamu akaoa Mkristo, lakini kila moja anafuata dini yake. Itakapofikia kwenye kuchinja! Mume atasema hali nyama isiyochinjwa na Mwislamu na mke naye atasema hali nyama iliyochinjwa na Mkristo, matokeo naona mjaze ninyi wenzangu.
Nakubaliana na kauli ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, pamoja na kauli ya Waziri Mkuu, kuwa utaratibu huo ubaki kama zamani tusianzishe mambo mengine ambayo yatatupeleka kwa majirani zetu kuwatenga wenzetu kwa ukabila na sisi kwa itakuwa kwa udini, viongozi hawa wa dini wanajua madhara yake.
Mwisho kabisa nawaomba viongozi hao wa dini watangaze neno la Mungu na wasibuni kutangaza mambo mengine ya dunia ambayo huenda utaratibu wake ulikuwepo toka zamani. Tena wakumbuke wosia wa baba wa Taifa hili Hayati Mwalimu J.K. Nyerere aliyosema Serikali ya Tanzania haina dini. Kila mtu anaweza kufuata dini aipendayo kwa imani yake, na siyo kusema dini hii masharti yake hayafai isipokuwa masharti mema ya dini hii nyingine. Naiomba Serikali pia kukemea jambo hilo maana litawagusa hata ninyi. Siku nyingine kutakuwa na dhifa ya kitaifa, mtaanza kubishana huko huko Mkristo atasema nyama hii kama imechinjwa na Mwislamu hali, na Mwislamu naye atasema kama haijachinjwa na Mwislamu naye hali matokeo mtajua ninyi chanzo kipo huko mwanzo.
Inashangaza viongozi wa dini wanashindwa kukemea Waumini ambao wanaonyesha vitendo vya aibu wanapofika kanisani baadhi ya akina mama hufika kanisani wakiwa wamevaa nguo ambazo ukweli zinaipotosha jamii. Nguo hizo wote tunazijua na sina haja ya kuzitaja mtindo unaitwaje kwa nidhamu yangu.
Mara nyingi mama hao huchelewa kufika kanisani kwa makusudi tu. Muda atakaofika huenda Padre au Mwalimu anatoa mafundisho (anahubiri) atakapoingia sisi sote macho kwake na kuacha kusikiliza mahubiri. Kitakachotustua ni mlio wa viatu vyake vyenye mithili ya miguu ya ngorombo. Ukiangalia mwili wake unatofautiana na alivyoumbwa na nywele pia. Kama utakaa jirani naye utapata kero ya harufu yake. Kwa vile nguo hizo sote tunazifahamu kweli ni vyema kuingia nazo makanisani au Msikitini? Ndiyo maana hapo mwanzo nimesema Mwislamu anavaaje? kwa nini hayo hamyasemi? Ni uchinjaji tu?
NB: Naomba viongozi hao wa dini (Hasa Maaskofu) wamwulize Papa Francis I ili tuelewe mageni na mapya haya ameleta yeye au ameyakuta mezani? Mwisho

Mzee Kapook Mkimbila
Mbilinyi wa Mkongotema - Songea
Muumini Wa Kanisa Katoliki
M / Tema

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jumuiya, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Abdurahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Muhammad Arif
Msambazaji: Mwl. Omar Mnungu
Wajumbe: 1. Abdullah Khamis Mbanga
2. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jumuiya Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu@yahoo.com

Bunge la Uingereza Lafanya Sherehe ya Kuadhimisha miaka 100 ya Ahmadiyya UK

Kutoka uk. 1

ya watu duniani kote, kwa hakika ni kuhusu suala la amani, upendo, usuluhishi ambao ni ujumbe wa kudumu, na endelevu kwa nyakati zote – miongoni mwa watu wa rika zote na jamii yote… Sote tunaungana nawe bila kujali rangi, tofauti za kiitikadi za vyama vya siasa au dini katika kusherehekea uwepo wa Jumuiya yenu hapa Uingereza kwa miaka mia moja lakini pia kusherehekea ujumbe ambao umeendelea kuenezwa na Jumuiya Ahmadiyya katika hali ya upole na heshima kuhusu - amani, upendo na usuluhishi."

Douglas Alexander, Katibu Kivuli wa Mambo ya Nje amesema:
"Katika dunia ambayo ina watu wenye tamaduni na changamoto nyingi, ujumbe huu wa usuluhishi unahitajika zaidi kuliko hapo kabla. Nataka ijulikane katika kumbukumbu kwa heshima kuwa tunatambua uongozi ambao wewe binafsi (Hazrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a) na jumuiya yako mmeuonesha, kwa kazi mliyoifanya, tofauti mliyoonesha na huduma mnayoendelea kuitoa sio tu kwa wanajumuiya Ahmadiyya bali kuwa sauti kubwa kwa ajili ya uvumilivu, usuluhishi na amani. 'Mapenzi kwa Wote bila Chuki kwa Yeyote' ni kauli mbiu ambayo sio tu twaweza kufaidika kwayo bali pia inatufunza mengi katika siku za usoni."

Mhe. Theresa May, Katibu wa Katibu wa Mambo ya Ndani amesema:
"Mtukufu (Hazrat Mirza Masroor Ahmad) ameonesha na anaendelea kuonesha kwamba njia pekee ya kukabiliana na watu wenye msimamo mkali ni mazungumzo ya amani. Huo ndio ujumbe ambao unautoa duniani kote na ni ujumbe ambao wote tunatakiwa tuusikilize na kuuzingatia. Nafahamu kwamba Jumuiya yenu imekuwa ikilengwa kwa mashambulio hususan nchini Pakistan ambako ni kosa la jinai kwa muahmadiyya kujiita Waislamu, na pia katika nchi hiyo Jumuiya Ahmadiyya imekuwa ikipata mashambulizi ya hatari. Kwa dhati kabisa nina nia ya kupambana na aina zote za itikadi kali popote zinapotokea … Nina uhakika kabisa kwamba katika miaka 100 ijayo kutakuwa na kundi la watu linaloadhimisha miaka 200 ya Jumuiya ya Waislam Ahmadiyya hapa Uingereza. Ninashukuru kwa kila mchango mlioutoa hapa Uingereza na sio hapa tu bali pia ninashukuru kwa ujumbe mnaoutoa duniani kote."



Kiongozi wa Jumuiya ya Waislam Ahmadiyya, Khalifa wa Tano, Hazrat Mirza Masroor Ahmad (a.t.b.a) akitoa hotuba katik-a hafla ya maadhimisho ya miaka 100 ya Jumuiya ya Waislamu Waahamdiyya Uingereza iliyofanyika chini ya Uenyeji wa Bunge la Uingereza.

Akitoa hotuba wakati wa hafla hiyo, Khalifa Mtukufu, Hazrat Mirza Masroor Ahmad (a.t.b.a) alizungumzia jitihada za Jumuiya ya Waislam Ahmadiyya katika kuendeleza amani na uvumilivu; alizungumzia umuhimu wa mtu kuwa mwaminifu kwa nchi yake kuwa ni sehemu ya imani. Huzur a.t.b.a alilaani vikali mauaji ya kinyama dhidi ya askari mmoja wa Kiingereza yaliyofanywa mjini London hivi karibuni. Khalifa Mtukufu a.t.b.a amepinga dhana ya Jihadi ya vita katika dunia ya leo na ametaka kuzingatiwa kwa suala la uadilifu katika jitihada za kuilinda dunia dhidi ya migogoro na vita.
Hazrat Mirza Masroor Ahmad (a.t.b.a) alianza hotuba yake kwa kuwahutubia viongozi wote wanaohusika na Kumbi za Bunge kwa kusema:

"Ni maombi na matarajio yangu kwamba idara zote na watu wote wanaofanya kazi katika jengo hili zuri na kongwe waweze kutimiza haki za kuhudumia nchi hii na watu wake. Aidha, ninamwomba Mwenyezi Mungu na ni matarajio yangu kwamba waweze kutekeleza majukumu yao katika namna bora katika kuendeleza uhusiano mzuri na mataifa mengine, kutenda kwa uadilifu na kufanya maamuzi ambayo yana manufaa kwa pande zote. Kama haya yatatekelezwa kwa ari hii, basi juhudi hizi zitazaa matunda mazuri ambayo ni mapenzi, urafiki na udugu na itafanya dunia kuwa pepo ya kweli ya amani na ustawi."

Hazrat Mirza Masroor Ahmad (a.t.b.a) alisema kwamba mtu kuwa mwaminifu kwa nchi yake ni sehemu muhimu ya dini imesisitizwa sana na Mtukufu Mtume Muhammad (S.A.W. Alisema kwamba Waislamu wote Waahmadiyya wanaoishi Uingereza wanayo shauku kuhusu "*maendeleo na ustawi wa taifa hili kubwa*." Aidha, Khalifa Mtukufu a.t.b.a aliipongeza Serikali ya Uingereza kwa kuwapokea wahamiaji wanaokuja Uingereza na kuwaruhusu kuwa "*sehemu ya jamii ya Waingereza*."

Khalifa Mtukufu a.t.b.a aliendelea kwa kusema kwamba katika kipindi cha miaka 100 ya uwepo wa Jumuiya ya Waislam Ahmadiyya Uingereza daima imekuwa ikihamasisha amani na kupinga aina zote za itikadi kali.
Hazrat Mirza Masroor Ahmad (a.t.b.a) alisema:

"Miaka 100 iliyopita imeonesha na kushuhudia kuwa wanajumuiya Ahmadiyya daima wametimiza sifa ya kuwa waaminifu kwa nchi yao na siku zote wameonesha kupinga aina zote za itikadi kali, vurugu na machafuko. Kwa hakika, sababu ya msingi ya uaminifu na mapenzi haya ni kutokana na ukweli kwamba Jumuiya ya Waislam Ahmadiyya ni Jumuiya ya kweli ya kidini ya Kiislam."

Kiongozi wa dunia aliendelea kwa kulaani na kupinga vikali dhana ya 'Jihadi ya vita au Jihadi ya kutumia nguvu'. Alikiri kwa masikitiko kuwa baadhi wale wanaojiita maulamaa wa Kiislam wamehamasisha mafundisho ya aina hii lakini kwa hakika wanapotosha na wanastahili kubeba lawama ya kuibuka kwa makundi mbalimbali ya kigaidi.
Hazrat Mirza Masroor Ahmad (a.t.b.a) alisema:
"Mfano wa hivi karibuni wa ugaidi kwa hakika ni yale mauaji ya kinyama ya askari wa Kiingereza asiye na hatia katika mitaa ya London. Ni shambulio ambalo halina uhusiano kabisa na mafundisho ya kweli ya Kiislam; badala yake, mafundisho ya Kiislam yanapinga kwa nguvu vitendo hivi."
Aidha, katika hotuba yake, Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alihimiza uvumilivu na kuheshimiana miongoni mwa waumini wa dini mbalimbali. Alisema kwamba Islam imeweka msingi wa amani kwa sababu Qurani Tukufu imefundisha kwamba manabii wa Mwenyezi Mungu walitumwa kwa watu na mataifa yote.
Hazrat Mirza Masroor Ahmad (a.t.b.a) alisema:
"Hakuna dini yoyote inayobainisha, kutambua na kuheshimu kila imani na kila taifa kama Islam."
Akielezea tabia ya kweli ya Mtukufu Mtume Muhammad (S.A.W), Hazrat Mirza Masroor Ahmad (a.t.b.a) alisema:
"Ni mwanzilishi wa Islam ambaye ametufanya tujenge mapenzi ya Mwenyezi Mungu na viumbe Wake katika nyoyo zetu. Ni yeye ambaye ametujengea mapenzi na heshima kwa wanadamu wote na dini zote. Mtukufu Mtume (S.A.W) alitumia muda wote wa maisha yake katika kueneza amani duniani. Hiyo ndio kazi yake bora. Kwa hakika, siku itawadia ambapo watu wa dunia hii watatambua na kuelewa kwamba yeye hakuleta mafundisho yoyote kuhusu itikadi kali. Watatambua kwamba mafundisho yote aliyoleta yalikuwa na ujumbe wa amani, mapenzi na huruma."
Akielezea kuhusu uhuru wa kidini kuwa ndio kanuni ya msingi ya Islam, Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisema:
"Kama moyo wa mtu unapenda basi yuko huru kukubali Islam, lakini ikiwa moyo wake haupendi, basi yu huru kukataa. Hivyo, Islam inapinga kabisa kutumia nguvu na itikadi kali; badala yake, inahamasisha amani na uelewano katika kila ngazi ya jamii."

Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alihitimisha kwa kuzungumzia kuhusu umuhimu mkubwa wa uwepo wa uadilifu katika dunia ya sasa. Alisema kwamba anahofia migogoro ya sasa inaweza kusababisha vita ya dunia iwapo aina zote za ubaguzi na ukiukwaji wa haki hazitakomeshwa.

Hazrat Mirza Masroor Ahmad(a.t.b.a) alisema:

"Kutokana na vitendo vya baadhi ya nchi, zipo dalili kwamba vita nyingine ya dunia inanukia. Kama vita ya dunia ikitokea basi Ulimwengu wa magharibi pia utaathirika sana kutokana na ukubwa wa vita hiyo na matokeo yake mabaya. Tujiokoe dhidi ya uharibifu wa namna hii. Tuokoe kizazi chetu kijacho kutokana na athari mbaya za vita. Ipo hatari kubwa ya kutokea kwa vita vya nyuklia. Ili kuepusha matokeo haya mabaya, lazima tushikamane na uadilifu, ukweli na uaminifu na tuungane pamoja kuyaondoa na kuyashinda makundi yote yanayotaka kueneza chuki na yanayotaka kuharibu amani ya dunia ."

Hafla hii ilikamilishwa kwa maombi ya kimya na baada ya hapo wageni walipata fursa ya kukutana ana kwa ana na Khalifa Mtukufu, Hazrat Mirza Masroor Ahmad (a.t.b.a).
Sherehe hizo za karne zilihudhuriwa nawaheshimiwa 68 wakiwemo wabunge 30 na wajumbe 12 wa Nyumba ya **Malodi** wakiwemo wajumbe sita wa Baraza la Mawaziri na Mawaziri wawili. Mashirika mbalimbali ya habari yakiwemo BBC, Sky TV na ITV pia yalikuwepo kutangaza tukio hilo.
Mapema kabla ya hafla hiyo viongozi watatu wa vyama vya siasa waliandika katika kile kinachoonekana kuwa ni kuunga mkono maadhimisho hayo ya karne. Akiipongeza Jumuiya ya Waislam Ahmadiyya, Mhe. David Cameron (MB), Waziri Mkuu wa Uingereza alisema Uingereza inajivunia kuwepo kwa Jumuiya Ahmadiyya na alimsifu na kumtaja Hazrat Mirza Masroor Ahmad kama "*mtu wa amani*."

Tafsiri ya kwanza ya Qur'an Tukufu kwa Kiyao yaona jua

Kutoka uk. 1

ingebidi niache kazi ya kuajiriwa (Serikalini) mara moja ili niweze kufanya kwa ufanisi kazi niliyokadhiwa. Hata hivyo Amir na Mbashiri Mkuu alinishauri nisiache kazi ambayo ilikuwa chanzo cha mapato ya kuendeshea maisha yangu. Niliukubali ushauri wake na hivyo nikaendelea na kazi ya kuajiriwa serikalini, wakati huo huo nikajitahidi kutafsiri Qur'an Tukufu, ingawa ni kwa kasi ndogo kama tutakavyoona hapo baadae.

Lugha ya kiyao.

Kiyao ni lugha ya kibantu na inakisiwa kuzungumzwa na watu takriban milioni mbili waliomo katika nchi za Tanzania (kusini), Msumbiji, Malawi na Zambia (Google-wikipedia).

Utaratibu wa kutafsiri.

Kulikuwa na masharti kadhaa ya kufuata wakati wa kutafsiri Qur'an Tukufu.

1. Tafsiri lazima ifanyike kwa kufuata tafsiri ya Qur'an Tukufu kwa lugha ya Kiingereza iliyoandaliwa chini ya usimamizi wa Khalifa Mtukufu wa Nne, Hadharat Tahir Ahmad (Rehema ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake).

2. Taarifa ya kazi ya kutafsiri ilitakiwa ipelekwe Makao Makuu ya Jamaat (Markaz) kila baada ya wiki mbili.

3. Anayetafsiri aingie mkataba na Jamaat wenye kuonyesha kuwa atafanya kazi hiyo kwa malipo (fedha) au la.

Masharti mawili hayakunipa taabu,lile la kufuata mwongozo wa Markaz katika kutafsiri na kuingia mkataba wa malipo au la, kwa kazi ya kutafsiri. Mimi niliamua kuingia mkataba wa kutolipwa fedha, bali nifanye kazi hiyo kwa kujitolea katika njia ya Mwenyezi Mungu. Hata hivyo tatizo langu likawa taarifa ya kila wiki mbili, kutokana na ukweli kuwa nikiwa afisa mwandamizi serikalini, kazi zangu za kiofisi zilikuwa nyingi na nilisafiri mara kwa mara. Kutokana na hali hiyo, kasi yangu ya kutafsiri ilikuwa ndogo mno kiasi kwamba wakati mwingine hakukuwa na kazi yoyote ya maana iliyofanyika ndani ya wiki mbili.

Kazi ya kutafsiri.

Kazi ya kutafsiri Qur'an Tukufu kwa Kiyao ilihusu kutoa mawazo/maana ya Qur'an Tukufu kutoka katika lugha ya Kiingereza kwenda katika lugha ya Kiyao. Bila shaka kazi hii ilihitaji umahiri katika lugha zote mbili.

Lugha ya Kiyao.

Mimi nilizaliwa (1950) katika familia ya wayao huko Chitandi, Newala, Mkoani Mtwara. Nikiwa mtoto mdogo (hadi miaka saba) nilipata bahati ya kuishi kwa karibu sana na babu yangu mzee Mosse (Che Mosse), ambaye nimeambiwa kuwa hadi kifo chake, alikuwa na umri wa takriban miaka mia moja. Yeye na mkewe (bibi yangu) wakati wote walizungumza kiyao na hivyo kuwa 'Shule' kwangu ya lugha hiyo, bila kujijua.

Lugha ya Kiingereza.

Kwa msaada wa Mwenyezi Mungu, nilipata bahati ya kusoma shule kwa muda mrefu na kupata astashahada, stashahada na shahada katika vyuo mbalimbali hapa nchini na nchi za nje (Uingereza). Lugha ya kujifunzia (ukiacha darasa la I-IV) wakati huo wote ilikuwa ni kiingereza, jambo ambalo limepanua uelewa wangu wa lugha hiyo.

Changamoto.

Kama nilivyokwisha dokeza, uchache wa muda wa kutafsiri Qur'an Tukufu wakati nikiwa mwajiriwa kilikuwa kikwazo kikubwa kwangu na hasa ukizingatia kuwa muda mwingi ulihitajika kwa ajili ya kusoma Qur'an mara nyingi kwa makini hususan sehemu husika, kabla ya kudiriki kutafsiri. Aghlabu aya moja niliitafsiri mara kadhaa na kwa nyakati mbalimbali. Hata hivyo mara nyingi sikuridhika nayo na nikaendelea kuitafakari na kujaribu tena kuitafsiri.

Katika mchakato huu wa tafsiri ndugu mbalimbali ambao ni wazungumzaji wa lugha ya kiyao akiwamo mke wangu Bi Khadija, walipata 'taabu' nyingi kutokana na majadiliano ya kina ambayo walilazimika kufanya nami kuhusu msamiati, semi mbalimbali, unyumbuaji wa maneno ya kiyao na kadhalika. Wengi waliniona ni mkorofi kwa hili na wakalazimika kuniomba tubadilishe mada katika mazungumzo yetu. Niliwaelewa kwani hata mimi nililazimika kuwaingiza katika zahama hiyo kutokana na kukosekana kwa vitabu vilivyoandikwa kwa lugha ya kiyao, ambamo ningalijifunza mambo mbalimbali kuhusu lugha hiyo.

Awali rasimu ya tafsiri niliiandika kwa mkono na kukawa na rundo la madaftari ya rasimu hiyo. Kwa msaada wa Mwenyezi Mungu baadaye Jamaat ikanunua computer kwa ajili ya kazi hiyo, Alhamdulillah.

Pamoja na hayo yote tatizo la kasi ndogo ya kazi ya kutafsiri Qur'an Tukufu kwa Kiyao, liliendelea kuwapo na likapelekea Khalifa Mtukufu wa Nne (Mwenyezi Mungu Amrehemu) kuniandikia barua mnamo Novemba 1998, akinieleza kuwa kwa kasi ndogo niliyokuwa nayo katika kazi hiyo, ingechukua miaka 750 kukamilika!. Alisema Jamaat isingekuwa tayari kusubiri kwa muda huo!

Kufuatia kauli hiyo ya Mtukufu Khalifa nilitafuta namna bora ya kuendelea na kazi hiyo adhimu. Hatimaye mnamo mwezi Mei 1999, niliamua kuacha kazi mara moja (Notisi ya saa 24) ili



Bw. Alli Saidi Mosse

nipate muda wa kutosha kwa ajili ya kazi hiyo.Naam uamuzi huo licha ya mashaka mengi ya kimaisha yaliyoambatana nao, ulinipa nafasi nzuri sana ya kuzama katika kazi ya kutafsiri usiku na mchana. Nililala na kuamka humo. Nikawa katika ulimwengu wa kwangu. Nilikuwa kana kwamba sipo Dar Es Salaam, ilhali ndiko nilikoendelea kuishi. Ushahidi wa kuendelea kuishi Dar ulipatikana Masjid Salaam, ambako nilionekana kila siku ya Ijumaa.

Aidha kufuatia uamuzi huo, kasi ya kazi iliimarika na hapakuchukua muda Markaz ikaniandikia barua yenye kuonyesha kuridhika kwao na maendeleo ya kazi niliyopewa. Bila shaka kwa upande mwingine mashaka yalikuwa makubwa kwa upande wa mke wangu Bi Khadija ambaye watoto wetu bado walikuwa shule ya msingi na yeye peke yake ndiye aliyekuwa akienda na kurudi kazini. Mimi nilikuwa kama nimegandishwa kwa gundi kwenye kiti na meza! Wakati wote kauli yangu ilikuwa '***tumuombe na kumtegemea Mwenyezi Mungu, ambaye ninaamini hatatuacha tuadhirike na kufa kwa njaa***' kwa sababu tu ya kujitolea katika njia yake. Usemi huu ndio uliotawala katika maisha yetu na kama nitakavyobainisha hapo baadaye, neema nyingi za Allah tumezi shudia.

Kwa msaada wa Mwenyezi Mungu kwa kadri kasi ya kazi ilivyoongezeka ndivyo pia msaada wa Mwenyezi Mungu katika sura mbalimbali ulivyodhihirika na kuondoa mashaka yaliyokuwepo hususan kwa Bi Khadija ambaye baadaye alinieleza mara kadhaa, kushangaa kwake kuhusu nafuu nyingi ambazo zilijitokeza bila kutazamia. Licha ya kutembelea maeneo mbalimbali, alipata fursa pia ya kwenda katika nchi ambayo Firauni alionyesha ufedhuli wake na akaangamia. Alituletea picha na maelezo ya jinsi mwili wa kiumbe huyo aliyekuwa na kibri kikubwa kwa Mwenyezi Mungu, ulivyohifadhiwa na kuwa kielelezo kwa vizazi vya baadaye.

Kutokana na kuongezeka kwa kasi ya kazi, nilifaulu kumaliza duru ya kwanza ya kutafsiri Qur'an Tukufu yote kwa Kiyao mwaka 2004. Baada ya hapo Mwalimu Rashid Yawali ambaye anajua lugha ya Kiyao, aliteuliwa na kukabidhiwa kazi ya kuipitia tafsiri yote na kutoa maoni yake. Masahihisho na maboresho mbalimbali kwenye rasimu ya tafsiri hiyo, yaliendelea kufanyika hadi kuchapishwa kwake 2013.

Baadhi ya neema tulizozishuhudia.

Bila shaka hakuna ambaye anaweza kuzihesabu neema za Mwenyezi Mungu (Qur'an Tukufu ……), lakini tuna wajibu wa kumshukuru Mwenyezi Mungu angalao kwa yale ambayo tumeyashuhudia. Ni kwa mnasaba huo ya kwamba ninaeleza kwa uchache hapa chini baadhi ya neema tulizozishuhudia.

Awali ya yote ni muhimu kufahamu ya kwamba kulikuwa na wasiwasi mkubwa kwangu na ndugu wengine pia kuhusu tafsiri ya Qur'an Tukufu kwa kiyao iliyokuwa inaandaliwa hapa nchini Tanzania kama ingeeleweka kwa wayao waliomo katika nchi zingine au la. Kwa msaada wa Mwenyezi Mungu kulikuwa na matokeo kadhaa yaliyopunguza kama siyo kuondoa wasiwasi huo.

Kwanza kabisa wakati nikitafsiri vitabu vitatu kwa kusaidiwa na wazee wawili kama nilivyokwisha eleza hapo juu, majadiliano makali yalifanyika baina yetu tukiwa kwenye jengo la 'Mission House' ambalo lilikuwa linajengwa kuongeza ghorofa moja. Mmoja wa mafundi wajenzi alikuwa myao kutoka Malawi. Baada ya kusikia majadiliano yetu hakuyaamini masikio yake na kwa hiyo alishuka chini akatuuliza tulikuwa tunafanya nini. Tuliimuuliza kama lugha tuliyokuwa tunaitumia anaielewa, naye akatueleza kuwa aliielewa vizuri na ndiyo maana akashindwa kuvumilia na hivyo akaja kwetu. Tulimsomea tafsiri ya Sura ya kwanza (Surat ul Faatiha), akatueleza kuwa aliielewa vizuri.

Halikadhalika mnamo miaka ya 1990, Chifu mmoja wa Wayao kutoka Malawi alihudhuria Mkutano wa mwaka (Jalsa Salana) wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya jliofanyika huko Morogoro. Katika salamu zake aliishukuru sana Jamaat Ahmadiyya kwa kuwapatia vitabu vya dini vilivyoandikwa kwa lugha ya Kiyao. Alisema kwa mara ya kwanza watu wake wamejua maana ya sura ya Alfaatiha.

Halikadhalika Mwalimu Hassan Mrope ambaye mara kwa mara alitumwa na Jamaat kwenda Msumbiji kuhamasisha shughuli za Jamaat, aliripoti kuwa vitabu vyetu vilifurahiwa mno na wazungumzaji wa lugha ya Kiyao na kwamba ilikuwa sababu ya watu kujiunga na Jamaat.

Kuhusiana na masuala ya maisha katika familia yangu, tumeshuhudia mengi. Lakini kwa neno zima ni kwamba tuliendelea kupata mahitaji yetu ya maisha na kwamba watoto wetu waliendelea vizuri na masoma. Vipande vya ardhi ambavyo tulifaulu kuvimiliki katika maeneo kadhaa ya Dar Es Salaam yaliendelea kupanda thamani na kuleta nafuu kubwa kwetu. Alhamdulillah.

Shukrani.

Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Ambaye Alitengeneza mazingira yenye kuniwezesha kufanya kazi hiyo muhimu. Isitoshe ninamshukuru kwa kunipa uhai nikaweza kuiona na kuisoma nakala ya Tafsiri ya Qur'an Tukufu kwa Kiyao baada ya kuchapishwa.

Ninawashukuru pia viongozi wa Jamaat hususan Khalifatul Masih wa Nne (Mwenyezi Mungu Amrehemu) na baadaye Khalifatul Masih wa Tano Hadhrat Mirza Masruur Ahmad (atb), ambao walifuatilia kwa karibu na kutoa msukumo hadi kukamilika kwa kazi hiyo.

Halikadhalika ninawashukuru na kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu awaweke mahali pema peponi wazee wetu waliotangulia mbele ya haki, Sheikh Issa Harun Karunguja na Mzee Karuma Issa, kwa 'kuninoa' katika lugha ya kiyao. Naikumbuka kauli ya Mzee Karuma Issa alipoteuliwa kusaidia katika kutafsiri kwa kiyao alisema 'Mimi ni mzee, huu ni mpango wa Mwenyezi Mungu wa kuniingiza peponi'. Na iwe hivyo kwa wote wawili.

Mwalimu Rashid Yawali naye anastahili shukrani kwa kazi nzito ya kupitia mswaada wote na kutoa mawazo yake kwa lengo la kuboresha Tafsiri.

Aidha namshukuru mno Mwalimu Abdulrahman Ame ambaye mara kadhaa tulikesha nae wakati wa kufanya masahihisho na kuandaa mswaada (Typesetting) kwa ajili ya uchapaji. Mwalimu Ame hakuwa anajua lugha ya kiyao na kwahiyo kazi ya kuandika kwa imla maneno marefu asiyoyajua maana yake ulikuwa mtihani tosha kwake. Sina uhakika kama baada ya 'mafunzo' yale ya lazima ameambulia chochote katika lugha ya Kiyao.

Aidha nina imani kubwa kuwa nimenufaika sana na maombi ya ndugu zangu wapendwa Waahmadiya wa rika na jinsia mbalimbali. Kwa wote mlipaji ni Allah.

Mwisho lakini si kwa umuhimu naishukuru sana familia yangu hususan mke wangu Bi Khadija kwa kuvumilia na kubeba mashaka yaliyoambatana na kazi hiyo. Polepole mashaka hayo yaligeuka kuwa kheri.

Mwisho.

Chapa ya kwanza ya tafsiri ya Qur'an Tukufu ipo tayari. Sote tumuombe Mwenyezi Mungu ili iwe yenye manufaa kwa wasomaji, hususan wale ambao hawana njia ya kulijua neno la Mungu isipokuwa kwa kupitia lugha ya Kiyao. Amin.

Kisa cha Nabii Issa (a.s.) Kusema Uchangani

Kutoka uk. 1

zilitangazwa na Nabii Isa (as) mbele ya wanafunzi wote ni kwamba aliitwa'Mwamba'. Na ikaahidiwa kwamba kanisa la Yesu (Isa as) lingejengwa juu yake. (Mathayo 16:18) huyu ndiye aliyekabidhiwa funguo za mbinguni (Mathayo 16: 19) ni jambo la ajabu kama itakuwa mtu mwenye sifa hizi ni mnafiki.

Yafaa tulitazame tukio hili kwa upana wake kabla ya kumhukumu Petro kwa unafiki.

leleweke ya kwamba Petro alikuwa ndiye mtu wa karibu mno na Nabii Isa (as) ikiwa kulikuwa na kiongozi wa wanafunzi wa Nabii huyu basi huyo atakuwa Petro. Ni mtu aliyekuwa na jazba kubwa ya imani. Ndiyo maana hata zilipovuma tetesi za Nabii Isa kutafutwa iii akamatwe na kusulubishwa, Petro ndiye aliyeahidi kuambatana na Nabii Isa (as) na hata ikibidi kufa pamoja naye (Mathayo 26:35). Na hata Nabii Isa (as) aliposema kuwa Petro atamkana mara tatu hakuwa akimaanisha kuwa atamsaliti. Hivyo kuna haja ya kujadili hadhi ya Petro kwa uangalifu na uadilifu.

Ikumbukwe kuwa pale barazani ulikuwa unatafutwa ushahidi wa kumtia hatiani Nabii Isa (as), alitakiwa apatikane mtu atakayemkiri Nabii Isa na madai yake iii ithibitike kuwa tayari aliishakuwa na wafuasi. Ndiyo maana wanafunzi wengine waliokuwa na udhaifu wa imani hawakuthubutu hata kutia mguu katika lile baraza, wote walitoweka (Marko 14:50). Angalau Petro alijikaza kiume na kubaki iii ashuhudie kadhia hii na hatima ya kiongozi wake mpendwa. Kwa hivi ilipofika zamu ya kuhojiwa juu ya uhusiano wake na Nabii Isa (as), alimkana siyo kwa kumkufuru, bali ilikuwa mbinu ya kukwepa kuwa shahidi wa Makuhani dhidi ya Nabii Isa (as).

Kwa ujumla tukio zima liliendeshwa katika hali ya vitisho na ubabe. Petro aligundua kuwa katika hali ile asingeweza kufanya lolote la kuweza kumsaidia Bwana wake. Ni wazi kuwa alipoahidi kuwa pamoja naye katika misukosuko hiyo hakuwa akifahamu hasa uzito wa kesi hiyo ulivyo. Ndiyo maana Nabii Isa alimtamkia kuwa pamoja na jazba aliyo nayo, jambo hili ni zito na litamfanya alazimike kumkana mara tatu.

Yawezekana kabisa katika tukio hili la Petro kumkana Nabii, ndipo ilipozaliwa ile dhana ya uongo mtakatifu - yaani kudanganya kwa nia ya kumwokoa mtu asiye na hatia.

Baada ya Petro kung'ang'ana kwamba hamjui Nabii Isa (as) bila shaka Makuhani walikosa mahala pa kushika katika jitihada zao za kutafuta ushahidi dhidi ya Nabii Isa (as).

Mwandishi maarufu wa historia ya Ukristo Dean Millman anaeleza kuwa hatimaye ndugu wa Nabii Isa (as) waliletwa katika baraza, baada ya kuteswa na kutishiwa kutengwa na jamii, walilazimishwa watoe ushahidi dhidi ya Nabii Isa (as). Lakini wote walijizuia kutamka lolote kumhusu Nabii Isa (as) iii kauli zao zisije kuchukuliwa kama ushahidi wa tuhuma hizo za uongo dhidi ya Nabii Isa (as). Wote walimwashiria yeye mwenyewe ndiye aulizwe juu ya taarifa zinazomhusu (tazama *History of Christianity* uk. 272).

Bila shaka aya za Qur'an Tukufu tunazozijadili zinarejea katika tukio hili. Kwa maana ni dhahiri ya kwamba Nabii Isa (as) alikuwa akitajwa kama mtu hatari miongoni mwa Wayahudi. Kauli na harakati zake zilielekea kuwatisha na kuwachukiza wakuu wa Kiyahudi. Hivyo walimhesabu kama mtu aliyehatarisha amani kwa jamii yao. Hii ndiyo mantiki iliyomaanishwa na kauli yao waliyoitoa kwa Mariyamu ya kwamba ameleta jambo lichukizalo. Kauli hii yaelekea kuwa ilitolewa baada ya Makuhani kuhenya katika kutafuta ushahidi na hoja dhidi ya Nabii lsa (as) bila mafanikio.

Hatimaye walimgeukia Mariyamu aliyeonekana kuwa bega kwa bega n a mwanawe katika sakata zima la kesi hadi kwenye tukio la msalaba. Kwa hivi, kwa maneno haya; "Ewe Mariyamu, bila shaka umeleta jambo lichukizalo". Hawakuwa wakimlaumu kwa kupata mwana nje ya ndoa, bali ni kule kuunga kwake mkono madai na harakati za mwanawe ambaye Wayahudi walimhesabu kama mhuni na mpinga dini yao.

Tuhuma za kuzaa nje ya ndoa hazikupata kutolewa dhidi ya Mariyamu, kwa kuwa inaonekana Wayahudi walikuwa wakiamini kwamba Isa (as) ni mtoto wa Yusufu Seremala (Luka 3:23, Mathayo 13:55) dhana hiyo inapata nguvu ikizingatiwa kwamba Mariyamu aliolewa na Yusufu kabla ya kuzaliwa kwa Nabii Isa (as), pia tukio la yeye kupata mimba kwa nguvu za Roho Mtakatifu halikuwa jambo Iililotangazwa hadharani.

Ndiyo maana hata aliyekuwa Mchumba wake, Yusuf hakujua hadi alipobaini kuwa mchumba wake ni mja mzito ndipo alipamua kumwacha kwa siri kabla hajabatilisha azma hiyo baada ya kujulishwa na Mungu kwa njia ya ufunuo. Kwa hiyo SHAI-AN FARIYYAH (Jambo Iichukizalo) hapa (kwa madai yao) ni kuamini unabii wa uongo wa mwanawe.

Ndiyo maana katika aya inayofuata, Makuhani wanaonekana kumrai Mariyamu, wakimliwaza kwa kumpa lakabu ya DADA WA HARUNI ikimaanisha kuutambua uadilifu wake, kwa maana Haruni ndiye mtu aliyeweka msingi wa Ukuhani katika Uyahudi.

Hivyo Wayahudi walimpa Mariyamu heshima ya kuwa dada wa Haruni kama njia ya kumtaka aungane nao na kuachana na madai ya mwanawe. Na wakasisitiza kwa kumkumbusha juu ya uchamungu wa wazazi wake.

Kwa kuwa Mariyamu alikwishaupokea ukweli wa Masihi alitaka mwanawe apewe nafasi ya kujieleza, na hivyo hakusema lolote bali aliashiria kwa mwanawe. Bila shaka alijua kuwa kama Nabii Isa (as) atapewa nafasi ya kusikilizwa, madai yake yangeweza kueleweka vyema mbele ya baraza liIe.

Lakini Makuhani wale, kama ilivyo suna ya Makafiri wote, hawakuwa tayari kusikia chochote kutoka kwa Nabii Isa (as). Na sawa na itikadi na kiburi chao, hawakuwa tayari kumsikiliza mtu waliyemzidi umri, bwana mdogo ambaye angeweza kuwa mtoto au mjukuu wao. Ndiyo maana hata mudamfupikablayakesikuanza kusikilizwa, Nabii Isa (as) alishaanza mahubiri palepale mahakamani. Alipozungumza jambo kumhusu Ibrahim (as), Makuhani walimkemea kwa kumwambia kuwa hajatimiza hata miaka 50 atazungumzaje juu ya Ibrahim (Yohana 8:57). Hii ndiyo maana hasa ya maneno "Tutazungumzaje na mtoto aliyepakatwa". Wakimaanisha kuwa huyu ni mtoto wa juzi juzi tu, hivyo kwa taadhima za Kiyahudi hakuwa na hadhi ya kuwahutubia Makuhani ambao aghalabu huwa na umri wa zaidi ya miaka 60. Hivyo kauli hii ilikuwa ni njia ya kumzuuia Nabii Isa asizungumze na kumng'ang'aniza Mariyamu ajibu.

HapaNabiiIsa(as)alishagundua mtego uliomzunguka mama yake. Alifahamu kuwa ukimya wake ungeweza kusababisha taabu na madhila makubwa kwa mama yake. Iii kumuokoa mama yake, aliamua kuhutubia baraza hilo bila kusubiri ruhusa ya Makuhani.

Wanahistoria wanaitaja hotuba aliyoitoa Nabii Isa (as) mbele ya baraza la Makuhani kwamba ilikuwa ni hotuba ya kihistoria, iliyojaa fasaha na umahiri mkubwa, hata baadhi wanaitaja kuwa ilikuwa ni hotuba iliyojaa hoja za kiwakili (tazama *Ecclesiastical History* uk. 201), Maelezo yanayokaririwa na Qur'an Tukufu katika aya hizi (19:30 - 33) ndiyo muhtasari wa hotuba hiyo.

Qur'an Tukufu imetaja nukta za msingi katika hotuba hiyo, kwamba Nabii Isa kwanza alithibitisha kuwa yeye ni Mtumishi wa Mungu, kisha akaelezea jinsi alivyopewa ufunuo wa Injili na kufafanua juu ya unabii wake. Katika hotuba hiyo pia alifafanua mafundisho yake kwamba hayakuwa na uhusiano wowote na harakati za kisiasa kama walivyomtuhumu, bali ameamrishwa kusimamisha sala na kutoa zaka, na kwamba amepewa jukumu kumsaidia mama yake. Qur'an Tukufu inahitimisha ukariri wake kwa nukta ya mwisho ya hotuba hiyo ambapo Nabii Isa (as) alithibitisha kuwa yeye si mtu mbaya na hatari katika jamii aliposema kuwa Mungu hakunifanya kuwa *JABBAARAN SHAQIYYA*.

Kwa haki hii ni wazi kuwa hoja hizi yumkini ziitolewa na Nabii Isa (as) akiwa mtu mzima aliyetimiza umri wa kuupewa majukumu. Hotuba hii iliyojaa fasaha na hoja zinazoingia akilini, kama ingetolewa na kichanga kilichopakatwa, bila shaka ingekuwa ni kioja cha kuogofya siyo tu kwa Makuhani bali hata mzazi wake na jamaa zake wa karibu wangetimua mbio na kuhamanika kwa mshangao.

=Mwisho=

Je Bwana Yesu kwa mujibu wa Biblia ni Mungu au La?

Bwana Yesu hajasema katika Biblia yeye aabudiwe.

Na Sheikh Ghulam Murtaza Dodoma

Siku hizi tunasikia kelele za watu wazushi kwamba Bwana Yesu ni Mungu kwa sababu ya sifa mbali mbali alizokuwa nazo sawa na Mitume wengine wa Israeli. Je tukubali maoni ya watu hao wazushi au tukubali maoni ya Bwana Yesu na maoni ya kitabu cha Mungu. Ndugu zangu; tunaposoma Biblia, tunapata maandiko kadhaa ambayo yanasema; Bwana Yesu alikataa itikadi hii inayoelezwa na watu wazushi kwamba yeye ni Mungu. Katika kitabu cha Yohana imeandikwa; Basi Wayahudi wakaokota mawe tena ili wampige. Yesu akawajibu, Kazi njema nyingi nimewaonyesha, zitokazo kwa baba; Kwa ajili ya kazi ipi katika hizo mnanipiga kwa mawe? Wayahudi wakamjibu, kwa ajili ya kazi njema hatukupigi kwa mawe, bali kwa kukufuru, na kwa sababu wewe uliye mwanadamu wajifanya mwenyewe u Mungu? Yesu akawajibu, Je Haikuandikwa katika Torati yenu ya kwamba, Mimi nimesema, Ndinyi miungu? Ikiwa aliwaita miungu wale waliojiliwa na neno la Mungu ... (YN,10-



Sheikh Ghulam Murtaza

31,33). Ndugu zangu maandiko haya yanafundisha wazi Bwana Yesu hakukubali kuitwa yeye ni Mungu, Bali sawa na mitume wingine aliwaita mwana wa Mungu.

(2). Katika kitabu cha biblia watu wengi wanaofanyakazi ya Mungu wameitwa wana wa Mungu. Katika kitabu cha Kutoka 4-22 kinasema; Nawe umwambie Farao, Bwana asema hivi, Israeli ni mwanangu mimi mzaliwa wa kwanza wangu; Sasa kila mtu mwenye busara anaweza kufikiria vizuri kwamba, kama ingekuwa nafasi ya mwanadamu awe Mungu au Mtoto wa Mungu basi Israeli alikuwa nafasi ya kwanza kabisa. Halafu Bwana Yesu alifafanua vizuri sana maana ya mwana wa Mungu. Aliposema katika Mathayo 5-9: Heri wapatanishi; maana hao wataitwa wana wa Mungu. Hao watu wazushi ambao kazi yao sio kupatanisha bali ni kupiga kelele hapa na pale nakujenga chuki tu; Je tufuate hao au Bibilia na Bwana Yesu.

(3). Tunaposoma Biblia tunaona Bwana Yesu alikuwa mtume wa Mwenyezi Mungu tu sawa na mitume wengine, Yeye alibatizwa. Katika Luka 3-21 tunasoma; Ikiwa watu wote walipokwisha kubatizwa na Yesu naye akabatizwa. Jamani kwanini siku hizi tunabatizwa, kwasababu tunakuwa na kasoro, na ndiyo sababu Bwana Yesu alipata ubatizo kwa mkono wa Yohana. Je inawezekana Mwana wa Mungu asili anahitaji kubatizwa? Kwasababu Mungu hana dhambi wala kasoro. Halafu Yesu hakukubali yeye ni mwema sembuse kusema yeye ni Mungu Marko 10-18 tunasoma: Yesu akamwambia, kwa nini kuniita mwema? Hakuna aliye mwema ila mmoja, ndiye Mungu. Hali hiyo

Endelea uk. 8

Bustani ya Washairi

ZANZIBAR HADI RUMI

Kwa fadhili za Allah ndugu zetu wa Zanzibar wamejaaliwa kupata kituo cha kumwabudia Mola wao. Mwl. Ame akienda sambamba na kauli ya Mtukufu Mtume s.a.w. isemayo: Kupenda nchi yako ni sehemu ya imani, ameimba beti hizi:

1. Ya Ilahi Ya Adhiimi, Upweke Mola Sattari,
   U Rahmani Rahiimi, Mfanyaji kila zuri,
   Hii Yako takrimi, tufanye wenye shukuri,
   Uliotupa maqami, ijaze Zanzibari,
   Izagae Yako Nuri, Zanziba hadi Rumi.
2. Palipo Umetuhami, mno umetusitiri,
   Kwa sujuda na qiami, tupafikie kwa ari,
   Izidi yetu fahami, wenyeji na muhajiri,
   Iliyopaa i'lmi, irudi Zanzibari,
   Izagae Yako Nuri, Zanziba hadi Rumi.
3. Zimepita Ayyaami, tukiomba kwa nadhiri,
   Walitaka kina ami, tuzikwe kwenye kaburi,
   Leo Mtoa hukumi, Keshasaini amri,
   Atakalo halikwami, lamea Zanzibari,
   Izagae Yako Nuri, Zanziba hadi Rumi.
4. Tujaze zako naimi, yavutie mandhari,
   Uzichonge zetu ndimi, tuonye na kubashiri,
   Kwa upole wa usemi, tusichoke kuhubiri,
   Mvua ya Ilhami, inyeshe Zanzibari,
   Izagae Yako Nuri, Zanziba hadi Rumi.
5. Ya Allahu ya Haliimi, Mletaji tadhkiri,
   Wanyonge bin Adami, Tuondolee kiburi,
   Kwa elfu kumi kumi, tuje kwenye hii kheri,
   Ya hakika Islami, ibaki Zanzibari,
   Izagae Yako Nuri, Zanziba hadi Rumi.
6. Tuishi kwenye nidhami, za Mtume desturi,
   Muhammad Mukhtami, tushike bila dosari,
   Waimarike Khuddami, wote kwenye msitari,
   Na zingine tandhiimi, zivume Zanzibari,
   Izagae Yako Nuri, Zanziba hadi Rumi.
7. Ni wengi walo watemi, hali dunia ghururi,
   Wajidhanio wasomi, kumbe mabingwa wa shari,
   Mbele ya zao shutumi, Mola Utupe saburi,
   Aliyonena Ghulami, yajiri Zanzibari,
   Izagae Yako Nuri, Zanziba hadi Rumi.
8. Nikubalie Karimi, niahidiyo haqiri,
   Mlangonipo sihami, ingashitadi hatari,
   Takimbia sisimami, kupaza hii habari,
   Waokoe arhami, itubu Zanzibari,
   Izagae Yako Nuri, Zanziba hadi Rumi.
9. Ya Ilahi ya Dawami, Iauni hii dari,
   Yalo makundi khasimi, Mola yape tadaburi,
   Hili shindo la rasimi, yote yatoke shuari,
   Na kisha kwenye uchumi, iponye Zanzibari,
   Izagae Yako Nuri, Zanziba hadi Rumi.
10. Ya Samiu Ya Aliimi, Mjuzi wa zetu siri,
    Mja wako Aslami, Mjazi na Mghufiri,
    Na sisi akina mimi, Ona tulivyo fakiri,
    Utusafishe tuhumi, tung'ae Zanzibari,
    Izagae Yako Nuri, Zanziba hadi Rumi.

Abdulrahman M. Ame, Dar es Salaam

MMEA

Mshairi mahiri wa Kiswahili hutokea akaimba ndege kumbe si ndege 'tuyuri'! Mshairi huweza kunung'unika kwamba pete yake imepotea. Na akina Jomo Kenyata wakaomboleza na kusema 'Jamani mpatie pete yake AbdulNassir'! Masikini wakandikaje pa nje penye mwanya hupaoni? Mnaitwa wazungupule. 'Utu busara' anataka busara zenu. Mistari ya Johari inahitaji lenu jibu, Tanganyika na Mvita jikumbateni matama. Na Unguja mnaitwa mmea huo, huo mmea gani? Ama kweli mtoto wa muhunzi asipofua - hufukuta!

1. Mmea uliopandwa, miaka kenda porini
   Shina lake likapondwa, na wanyama wa mwituni
   Matawie yakadandwa, na ngedere kwa manyani
   Huu ni mmea gani, usokufa kwa shurubu?
2. Wakaalikwa wapambe, wenye maguvu mwilini
   Wakayabeba majembe, na masururu begani
   Wakataka wauchimbe, upotee aridhini
   Huu ni mmea gani, usokufa kwa shurubu?
3. Mmea ukasitawi, wachukie wahaini
   Walipolikata tawi, yakachipua sabini
   Mmea hautakiwi, japo waleta husuni
   Huu ni mmea gani, usokufa kwa shurubu?
4. Wakautupia kago,ufutike ramanini
   Mmea huu kigogo, watamba ulimwenguni
   Abadani si muhogo, si mtende wa jangwani
   Huu ni mmea gani, usokufa kwa shurubu?
5. Swila mchiriza sumu, nitoe tongo machoni
   Wa mamba kungwi walimu, mvumilika wa pwani
   Ya mashairi kaumu, na Wamwera nijibuni
   Huu ni mmea gani, usokufa kwa shurubu?

Lutufu A.Mbanga (Utu busara)
S.L.P 1 MOROGORO. SIMU: 0655 133337
Barua pepe:lutufumbanga@gmail.com

UNAKUWAJE HAKIMU?

Haihata haihata - kuwatumikia mabwana wawili. Mshika mbili moja si yake. Kazi ya uhakimu uwaachie watu wengine. Au wenzio utatupa kicheko!

1 Wewe mlalamikaji, unakuwaje hakimu?
Ni jambo katu haliji, kuipitisha hukumu
Wa vijijini na miji, waamba hiyo haramu
Unakuwaje hakimu, kumbe mlalamikaji?

2 Kumbe mlalamikaji, mwenzio wamshutumu
Vipi upewe siraji, kumulika humuhumu
Hiyo kazi ya miraji, wewe ukae sehemu
Unakuwaje hakimu, kumbe mlalamikaji?

3 Kaditama nataraji, utafuata nidhamu
Kutumia lako taji, wengine kuwadhulumu
Utajasombwa na maji, ja Firauni kaumu
Unakuwaje hakimu, kumbe mlalamikaji?

Mahmood Hamsin Mubiru (Wamamba)
Dar es Salaam

FADHAKIRI USICHOKE

Kukumbusha ni agizo la Kahari. Tukumbushane. Na hakuna lililo la kheri kuliko ujaji wa Mtume wa Allah. Amedhihiri tayari. Hatuwezi kukaa kimya. Kesho tutaulizwa. Ukimya unafaa tu kwenye ulimi wa kondoo na sio Mwaminio. Msikilize vizuri 'Siasa' Ukishaelewa tekeleza, kwani kwetu njia ni moja tu - 'Sami'na wa A'twa'na' (Tumesikia na kutii).

1. Waiteni watu wale, mbona wangali baidi,
   Wamekaa pale pale, wanamngoja arudi,
   Yule alokwenda kule, aloitwa na Wadudi,
   Fadhakiri usichoke, askari wa Mahadi.
2. Wangali kwenye ukale, zama zao Wathamudi,
   Wanasoma chuo kile, cha ngano za Namrudi,
   Chao wametupakule, wamebaki na nyiradi,
   Fadhakiri usichoke, askari wa Mahadi.
3. Hujiona wateule, kwa mavazi na jasadi,
   Hupenda viti vya mbele, julusi za Masayidi,
   Wao hawaweki mbele, dini hii ya Wadudi,
   Fadhakiri usichoke, askari wa Mahadi.
4. Wakumbushe watu wale, siku nyuma hazirudi,
   Na mwendowe ni wa pole, sio joto si baridi,
   Mwambie huyu ni yule, Masihi wa Muhammadi,
   Fadhakiri usichoke, askari wa Mahadi.
5. Japo zipigwe kalele, za kupasua fuadi,
   Kwa vinubi na kengele, au sauti za radi,
   Hayo yasikupe ndwele, kwenye yako makusudi,
   Fadhakiri usichoke, askari wa Mahadi.
6. Leo huku kesho kule, wapelekee Mahadi,
   Wendee kule kule, sifaze kwenda zinadi,
   Usiogope vitale, kwa kazi yake Majidi,
   Fadhakiri usichoke, askari wa Mahadi.
7. Sifa zake mteule, Sayidina Ahmadi,
   Katu hazitaki shule, bali imara fuadi,
   Na upendo wa milele, Walidi na Auladi,
   Fadhakiri usichoke, askari wa Mahadi.
8. Kule Qadiani kule, aliko zawa Sayidi,
   Kule lilitoka lele, huku ikashuka radi,
   Adhana zi teletele, misikiti na junudi,
   Fadhakiri usichoke, askari wa Mahadi.
9. Ndipo nasema tawile, kwa Mtume Muhammadi,
   Kutaja hadithi zile, za ujaji wa Mahadi,
   Yu Khalifa mteule, Rasuli na Mujadidi,
   Fadhakiri usichoke, askari wa Mahadi.
10. Sasa najibanza kule, Mikila bado mweledi,
    Zile vita za mishale, katu leo si jihadi,
    Jihadi sasa ni ile, kumhimidi Wadudi,
    Fadhakiri usichoke, askari wa Mahadi,

Ustadhi: A.R.Mikila (SIASA) Morogoo 10-April 201

MIHADHARA IMEFANA

Na njia bora ya kukumbusha ni mihadhara. Profesa hakuna alichoacha. Tangu lini Profesa akaacha kitu. Kachora Taswira na kwa jicho la ubongo tunawaona waliokusanyika. Tunamuona Kaluta, Karimu ud Dini, Asif na Kungwi wakigawa mali. Twaeni mali hii enyi waja wa Rabbana. Linalowezekana leo kwa nini mngoje kesho?

1. Ahamadiya hakika, mihadhara imefana,
   Kila ilipofanyika, ilikuwa raha sana,
   Watu wengi walifika, wazee pia vijana,
   Mihadhara imefana, Moro imetia fora.
2. Tumefanya Sangasanga, walofika wameona,
   Mindu kule kwa wahenga, hako aliyetuguna,
   Kidini tumewajenga, hawadanganyiki tena,
   Mijadala imefana, Moro imetia fora.
3. Mafisa nako kwa Mambi, kadhalika na kwa Sina,
   Kote tulipiga kambi, kama Jalsa Salana,
   Wakajua kumbe dhambi, zina urefu wa kina,
   Mihadhara imefana, Moro imetia fora.
4. Msamvu kwa ndege wengi, mbele ya wajahidina,
   Tuliwapa mambo mengi, yahusuyo Subuhana,
   Vile vile na misingi, ya kuwa waswalihina,
   Mijadala imefana, Moro imetia fora.
5. Mwembesongo Mji mpya, Kaloleni tumetuna,
   Mlapakolo sawiya, kwa Kairo tumevuna,
   Kweli ya Ahamadiya, ndipo ikaonekana,
   Mihadhara imefana, Moro imetia fora
6. Mijadala ikakuza, kwa marefu na mapana,
   Tukawaondoa giza, nuru ikaonekana,
   Wakamwelewa Mirza, Mteule wa Rabbana,
   Mijadala imefana, Moro imetia fora.
7. Mirza ndiye Masihi, kipingamizi hakuna,
   Ni Khalifa mwenye dhihi, anaongoza safina,
   Apaswa tumsitahi, kwa nguvu za Maulana,
   Mihadhara imefana, Moro imetia fora.
8. Jingine wamelikiri, Roma na Angilikana,
   Kazikiwa Kashimiri, Yesu huyo wao Bwana,
   Kaburi lake dhahiri, picha yake waliona,
   Mijadala ilifana, Moro imetia fora.
9. Kaluta alitanzua, hoja zote kwa bayana,
   Macho aliwafumbua, kwamba leo sio jana,
   Na pia mwezi na jua, siku moja hupatana,
   Mihadhara imefana, Moro imetia fora.
10. Akaja Karimudini, na hoja safi mwanana,
    Naye Asifu wa shani, akaziondoa dhana,
    Ikavuma tafurani, Mbanga alipowabana,
    Mijadala imefana, Moro imetia fora.
11. Tuitafute elimu, Mwenyezi Mungu Kanena,
    Tuupate ufahamu, akili zisende kona,
    Madarasa ni muhimu, ndio chanzo cha hazina,
    Mihadhara imefana, Moro imetia fora.
12. Hii mihadhara yetu, tunaifanya kwa mana,
    Tumche Muumba Wetu, tutukuze Lake Jina,
    Ugomvi si lengo letu, Wahamadiya hatuna,
    Mijadala imefana, Moro imetia fora.
13. Beti hizi namaliza, Amina Rabbi Amina,
    Tutazidi iongeza, mihadhara kila kona,
    Na amani kuikuza, fujo tuzipige lana,
    Mihadhara imefana, Moro imetia fora.

Professor: Kamdulla Msimbe,
Ahmadiyya Muslim Jumuiya,
S. L. Posta, 1 Morogoro.

NDOA

Haipendezi kufanya masikhara na ndoa. Na kumbuka ndoa sio ndoano. Nusu ya dini inapatikana katika jambo hili. Utalifanyiaje mchezo na masikhara? Lakini ndoa inaambatana na kanuni. Na nani wa kuzieleza kanuni hizo? Kuliko Kungwi? Ama kweli pumu imempata mkohozi!

1. Ndoa jambo la maana, wahenga walitongoa
   Ni suna ya Sayidina, kuoana ni kikoa
   Si pingu ya kufungana, mushindane kuitoa
   Ndoa ndoana si ndoa, ndoa ni kufungamana
2. Ndoa eti ni ndoana, majuhali huzogoa
   Suna wanaitukana, la kheri wanabomoa
   Sure wanadanganyana, mila kuimomonyoa
   Ndoa ndoana si ndoa, ndoa ni kufungamana
3. Ndoa ikiwa ndoana, ni uvuvi wa kuloa
   Na iwapo chambo huna, huolewi na kuoa
   Nikahi si kuvuana, kwa papa na changudoa
   Ndoa ndoana si ndoa, ndoa ni kufungamana
4. Ndoa ni kuchaguana, ndoana hozoazoa
   Wenza ni kuelewana, maadui kuzodoa
   Ya mishipi kutegana, si ndoa twaikosoa
   Ndoa ndoana si ndoa, ndoa ni kufungamana
5. Ndoa kusuhubiana, kwa khilafu kuondoa
   Bibi bwana kushikana, maisha kuyaongoa
   Na siyo kupelembana, kama pweza kuchokoa
   Ndoa ndoana si ndoa, ndoa ni kufungamana
6. Ndoa kukubaliana, muolewa na muoa
   Si vigongo kulengana, cha embe ya kupopoa
   Au kulazimishana, vya haramu kupochoa
   Ndoa ndoana si ndoa, ndoa ni kufungamana
7. Ndoa maizi kizama, maishani mtapoa
   Mdumu kwa kuengana, na kuliliana ngoa
   Kamwe hatopatikana, wa ndoani kuwang'oa
   Ndoa ndoana si ndoa, ndoa ni kufungamana
8. Ndoa mkiliwazana, uchovu mtaondoa
   Na hasa mkipendana, hunoga yanayoboa
   Mwaweza saidiana, kuoga hata kunyoa
   Ndoa ndoana si ndoa, ndoa ni kufungamana
9. Ndoa mkishashibana, hila mtazikomoa
   Mkiridhi visonona, mule pasi kujigoa
   Ndiko kuheshimiana, kunakodumisha ndoa
   Ndoa ndoana si ndoa, ndoa ni kufungamana

Abdullah Hamisi Mbanga (Kungwi)
Tambani - Mkurungana Pwani

Semina ya Ansarullah Kagera yafana

Na Mwandishi wetu

Tanzimu ya Majlis Amila Answarullah Taifa chini ya uongozi wa Sadr wake Muadhamu Inayatullah Seif Nakuchima sahib, mwaka huu wanakusudia kufanya Semina nne ambazo zitakuwa sehemu mbalimbali ya nchi yetu. Madhumuni ya Semina hizi ni kuwapatia elimu na uelewa mpana viongozi wetu wa matawi, Mikoa na Kanda ili angalau waweze kufahamu namna ya mfumo wa uongozi na majukumu yetu. Lakini vile vile juu ya namna na jinsi ya kufanya Tajnid (Sensa) yetu. Ni katika Semina hizi viongozi wanafundishwa namna ya kuchukua Bajeti na huelimishwa pia namna ya kuendesha vikao na umuhimu wao kuandika Taarifa katika kila ngazi.

Mwaka huu, hadi sasa semina moja tayari imeshafanyika kule Bukoba Kagera mnamo tarehe 16 na 16 Juni 2013. Kutoka Makao Makuu, Tanzimu ilipeleka viongozi 5 wakiongozwa na Naib Sadri Saf Awwal Bwana Abdullah Bin Nasoro. Viongozi hao wakati wanaenda Kagera kwenye semina hii waliazimia kulala Msikitini kwa siku zote mbili, kumbe wanyeji wao walikwisha andaa nyumba maalumu ya kufikia wageni wao. Alhamdulillah Allah Awajazi kheri na baraka tele.

Naam, tarehe 15/06/2013 kikao cha kwanza cha semina kilianza mnamo saa 2:45 hadi saa 7 mchana. Kwa ajili ya ufunguzi, kikao cha kwanza kiliendeshwa na Naib Sadri Awwal, nacho kilianza kwa usomaji wa Qur'an Tukufu iliyosomwa na ndugu Abdi Bishazo. Alisoma sura 24 toka aya ya 52 hadi 58 ambamo ndanimwe mna aya inayotupa neema kubwa ya Ukhalifa, nyingine imetuagiza tuwe watii. Wakadhalika katika aya hizo waaminio wameelezwa pia umuhimu wa kuswali na ulazima wa kutowa mali katika njia ya Mwenyezi Mungu kama vile Zaka na sadaka. Baadae kulisomwa shairi la beti tano na Bwana Hassani Ndatama ambaye ni Nazim wa Mkowa wa Mwanza. Kwa ruhusa ya Mwenyekiti, alisimama sasa Bwana Salum D. Mtamila ambaye ni Naib Sadri wa II kwa kufunguwa Semina kwa kusoma khutuba ya Sadri Sahib mwenyewe ambaye kwa sababu isiyozuilika hakuwapo kwenye semina hii.

Katika Khtuba hiyo, Sadri Sahib aliwashukuru wale Answarullah waliohudhuria kwenye Semina hii kwa kuacha nyuma yao watoto na shughuli zao za kujipatia riziki. Alisema, huko ndiko kutanguliza dini. Khutuba hiyo pia iliwakumbusha wanasemina kwa kuwaambiya kwamba utaratibu wa kuwapatia semina viongozi wetu utaendelea mpaka pale patakapoonekana kila Mwana Answarullah ameiva barabara katika kuitumikia Tanzimu na Jumuiyya kwa ujumla. Tutaendelea kumwomba Khalifa Mtukufu kutupatia nafasi hii.

Sadri sahib katika Khutuba yake hiyo iliyosomwa na Sadri wa II Bwana Mtamila alisema pia kuwa toka mwaka 2008 semina kama kumi na moja hivi zimefanyika. Akazitaja, nazo ni; Kanda ya Kusini hadi sasa semina 4 zimefanyika. Dar es salaam 3 na Mkoa wa Morogoro mara 2. Pwani na Iringa mara moja-moja. Lakupendeza ilisema Khutuba hiyo, kila sehemu iliyopita semina hii, kwa kweli kumeacha athari kubwa sana. Viongozi wetu wa ngazi tofauti na wanachama wa Tanzimu yetu wanaelewa nini wajibu wao.

Sadri Sahib amewahimiza na kuwapa nasaha, si wanasemina hiyo tu, bali kwa Answarullah wote kwamba ni wakati muafaka sasa kuitanguliza dini kuliko kitu kingine chochote. Tutowe kwa wingi bila kujali umaskini, kwa sababu pamoja na dhiki ipo faraja. Tukifanya hivi, Mwenyezi Mungu Atatusogezea baraka za aina aina na fadhila zake katika makazi yetu. Ilimalizia khutuba ya ufunguzi wa semina.

Baada ya khutuba hiyo ya ufunguzi wa semina, Wana Answarullah wasiopunguwa 19 waliingia rasmi kwenye masomo yaliyokusudiwa. Katika kikao hiki cha kwanza, wanasemina walifundishwa masomo mawili tofauti. Bwana Ramzan Fazal ambaye ndiye Mkufunzi wetu Mkuu aliendesha mada juu ya mfumo wa Uongozi na majukumu yetu. Mada ya pili iliwakilishwa na Bwana Abedi Idi ambaye ni Nazim pia wa Mkoa wa Dar es salaam. Yeye alielimisha wanasemina juu ya Tajnid (Sensa) somo ambalo halijafahamika vizuri kwa wanachama wetu wengi. Mpaka hivi sasa hatujawa na hesabu sawasawa iliyokamilika. Hesabu tuliyonayo ni ya miaka mitatu iliyopita.

Kikao cha pili kilianza saa 8:45 hadi saa 11:30 jioni. Kwenye muda huo, wanasemina walifundishwa namna ya uendeshaji wa vikao vyetu vya Tanzim. Mwalimu wa somo hili kama kawaida alikuwa Mkufunzi Mkuu Bwana Ramzan Fazal. Kisha wanasemina wote kwa pamoja walishiriki kwenye somo la vikao vya mfano.

SIKU YA PILI

Tarehe 16/06/2013 semina iliendelea chini ya uongozi wa Naib Sadri Saf Awwal Bwana Abdullah Bin Nasoro. Hiki kilikuwa kikao cha tatu ambacho kilianza saa 2:45 na kuendelea hadi saa 6:30 mchana. Nacho kilianza na usomwaji wa Qur'an Tukufu kisha palisomwa shairi. Baadaye wanasemina waliingia kwenye somo zito la Bajeti. Somo la kuchukuwa Bajeti lilifundishwa na Mtaalamu Bwana Hemedi Sheikh Ubwa ambaye ni Qaid Umumi wa Taifa kwa niaba ya Qaid Mal. Somo la pili lilikuwa juu ya fomu ya ufuatiliaji wa michango, somo ambalo liliendeshwa na Bwana Abedi Idi.

Kikao cha nne ambacho ndicho kilikuwa cha mwisho kilianza mnamo saa 8:30 mchana kwa usomaji wa Qur'an Tukufu kama kawaida. Ilisomwa sura ya 77 toka aya ya 1 mpaka 16. Ni aya ambazo zinaeleza shughuli mbalimbali zinazotendwa na pepo na hali halisi itakavyokuwa akheri zamani. Kisha Bwana Salum D. Mtamila ambaye ni Naib Sadri wa II alikuwa Mwalimu wa s omo la umuhimu wa Zaim kutayarisha na kuandika taarifa yake ya shughuli ya Tanzimu na kuipeleka kunako husika. Hili ndilo lilikuwa somo la mwisho katika semina hii ambayo ilichukuwa muda wa siku mbili.

KUFUNGA SEMINA

Kabla hajamkaribisha mgeni rasmi ili aje afunge semina, Naib Sadri Saf Awwal bwana Abdullah Nasoro alikuwa na maneno machache kwa wanasemina. Kwanza aliwashukuru wenyeji waliochukuwa uzito wa kukubali semina ifanyike kwao. Pia aliwapongeza wanasemina wenyewe kwa namna walivyohudhuria masomo hayo kwa bashasha na kuyafurahia, kadhalika aliwashukuru waalimu wote walioendesha semina hii hadi ikafana kwa kiasi kikubwa. Kwa wanasemina wenyewe, Sadri aliwataka watakapokuwa matawini mwao wayatumie yale yote waliyojifunza hapo ili Tanzim iweze kufanya kazi kwa uhakika na kupata maendeleo.

MGENI RASMI AFUNGA SEMINA

Mgeni rasmi aliyefunga semina hhii alikuwa Mbashiri wa Mkoa wa Kagera Mwalimu Khalifa Rashidi Mahovera ambaye naye alisisitiza umuhimu wa kutanguliza dini juu ya dunia. "Ninyi Answarullah, kwa kweli mna wajibu mkubwa sana na sawa kama mtaitikia kwa vitendo kwamba mu wasaidizi halisi wa Allah". "Mimi" alisema Mwalimu Khalifa, "ni (kijana) Khuddam, lakini mmenialika nije niwafungieni semina yenu hii. Ninamshukuru Mola kwa hilo, lakini nasema kwamba yale yote mliyojifunza hapa yachukueni mkayafanyie kazi kwenye matawi yenu. Nina hakika", akikazania kauli yake, "Iwapo kila mmoja wenu atatekeleza yale yote aliyochota hapa, basi mkoa wetu wa Kagera utasonga mbele bila wasiwasi". Mwisho aliwashukuru Wakufunzi wa Semina hii kwa kazi nzuri waliyoifanya. Bali alimshukuru zaidi Sadri Sahib kwa kukubali semina hii kufanyika Mkoani Kagera.

MAONI YA WANASEMINA

Kulikuwapo na maoni ya wanasemina pia. Mzee Abdulrahman Nyamihasi alionesha furaha yake kubwa sana aliyokuwa nayo juu ya semina hii kufanyika Mkoani kwao. Alisema semina hii kwa hakika imeimarisha na kukomaza imani yao, si kwa Tanzim tu, bali kwa Jumuiyya kwa jumla.

Bwana Habibu K. Issa kutoka Karagwe alifurahishwa mno namna masomo ya semina yalivyoendeshwa. Alisema kwamba kwa kweli wamefumbuliwa macho juu ya mambo mbalimbali na sasa wanajuwa waanzie mahala gani.

Bwana Abdi Bishazo alitamka wazi kwamba mambo waliyojifunza hapo hawakuwa wanayajuwa hapo kabla. "Semina", Bishazo alisema "niliiona kama muujiza vile kutoka mbinguni". Alimmiminia pongezi Sadri sahib Muadhamu Bwana Inayatullah S. Nakuchima kwa juhudi zake anazoonesha katika kuzagaza shughuli za Tanzim nchini.

Bwana Hamdani Athumani wa Katoma kule Bukoba alisema kwamba pamoja na masomo ya semina yalikuwa magumu kwa upande wake, lakini amenufaika sana. Amepata mwanga wa kutosha wa kumwezesha yeye naye kuuwasha tawini kwake. Ni baadhi tu ya maoni ya Answarullah 19 waliohudhuria semina ya Tanzimu kule Bukoba mkoani Kagera.

=Mwisho=

Tuangalie Michango Yetu

Ndugu Answarullah, tuangalie juu ya utoawaji wa michango yetu mbalimbali. Taarifa sahihi tuliyo nayo ni kuwa wana Answarullah wachache sana ndiyo wanaoshiriki katika zoezi hili kila mwezi bila kuchoka. Kuna wanaotowa nusu nusu, mwezi huu wanatowa mwezi mwingine hawatowi, wapo wengine ambao ndio wengi zaidi hawatowi chochote.

Enyi Answarullah, mjuwe kwamba Tanzim yetu inajitegemea kwa kila kitu. Hatuna mfadhili yeyote ila tunategemea michango ya kila mmoja wetu. Michango itakayotolewa na sisi sote, ndiyo kichocheo cha kuendesha shughuli zetu zote. Mapato yetu ya fedha si mazuri, hayaridhishi hata kidogo. Tuko chini sana. Angalieni, hata Bajeti yetu ya mwaka haifiki milioni 15. Tuko nyuma mno na ni lazima kila mmoja wetu ahakikishe anatowa michango yake bila kukosa. Tuna mengi ya kufanya tukiwa kama Tanzim. Tunashindwa kuyatenda hayo kwa sababu wanachama wetu wengi hawatilii manani umuhimu wa kutowa michango ya kila mwezi. Wale walio wakulima baada ya mavuno yao wanasahau kutowa michango yao. Imekuwaje?

Kila Mwana Tanzimu wetu afahamu kwamba jukumu la kuendeleza maendeleo ni ya kila mmoja. Uongozi wa kitaifa unapenda sana kuendesha semina kwa wanachama wake Mikoani na hapa Makao Makuu pia. Hali inabana, fedha za kugharamia kazi hiyo hatuna. Tunataka kuchapisha vipeperushi vyenye maudhui mbalimbali tunashindwa kwa minajili ya mkononi hatuna chochote. Zipo kazi nyingi za Tanzimu zinatakiwa zifanywe, lakini hazifanyiki kwa sababu ya ukwasi.

Kwa namna hiyo, ni wakati muafaka kwa Ansarullah wote sasa kukaa sawa katika nidhamu ya kutowa michango yetu bila kusahau bila kuchoka. Hapa mbele yetu kuna Ijtimaa. Ni wangapi kati yetu hadi sasa wametimiza kutowa zile shilingi 5,000/= tulizokubaliana? Huenda wakawapo hao, basi tunawakumbusha kwamba siku zilizosalia ni chache mno. Ni vizuri mchango wako ukatowa sasa. Allah Atusaidie sote. Amin
Juwa uwekacho ni cha wenzio
Na unachokula fahamu ni choo
Zaka na sadaka kwako ni ngao

WABILLAHI TTAUFIQ
MAJLIS ANSWARULLAH TAIFA
DAR ES SALAAM

Hadhrat Khalifatul Masih V a.t.b.a aidhinisha Majlis Amila Mpya (2013 - 2016)

Kufuatia uchaguzi wa wajumbe wa Majlis Amila Taifa uliofanyika wakati wa Shura ya Kitaifa iliyopita, Amir Jamaat Tanzania anapenda kuwaarifu Wanajumuiya wote nchini kwamba Hadhrat Khalifatul Masih a.t.b.a. ameidhinisha majina ya ndugu wafuatao kuwa wajumbe wa Majlis Amila Taifa kwa kipindi cha 2013/2016.

Amir Sahib anawaombea ndugu hao utendaji mwema wa majukumu yao. Amin.

Na.	WADHIFA	JINA
1	Katibu Mkuu	Seif Hassan Nakuchima
2	Katibu wa Maal	Ramadhani Hassan Mrope
3	Katibu wa Tabligh	Ali Khamis Mbambwa
4	Katibu wa Tarbiyyat	Mahmood Hamsin Mubiru
5	Katibu wa Taalim	Dr. Kitabu Salehe Pazi
6	Katibu wa Ishaat	Jamil Iddi Mwanga
7	Katibu wa Waqfe Nau	Fadhili Ali Namkumbe
8	Katibu wa Tahrike Jadid	Amiri Abedi Kaluta
9	Katibu wa Waqfe Jadid	Fadhili A. Mikila
10	Katibu wa Jaidad	Daud Daniel
11	Katibu wa Sami Basri	Aziz Ahmad Ngamilo
12	Katibu wa Dhiafat	Abdallah Jaffar Msesemele
13	Katibu wa Umure Amma	Dr. Mahadhi Mmoto
14	Katibu wa Ziraat	Alli Saidi Mosse
15	Katibu wa Sanatu Tijarat	Yusuf Shaban Malinda
16	Katibu wa Wasayat	Ramzan Fazal Madhani
17	Katibu wa Rishta Nata	Salum Dadi Mtamila
18	Katibu wa Maal wa ziada	Mwl. Omar

Sheikh Muhammad Arif Bashir
KAIMU AMIR
AHMADIYYAMUSLIMJAMAATTANZANIA

DUNIA -I-MAZIGAZI TUNAELEKEA WAPI HIVI SASA?

Na Khamisi Wamwera -
Dar es salaam

Mnamo tarehe 18 Oktoba mwaka 1981, Hadhrat Amirul Muuminina Khalifatul Masihi III, katika khutuba yake ya Ijumaa alitamka; "Wanadamu wanasogelea kwenye maangamizo makubwa yenye kutisha na matokeo hayo mabaya sana yameanza kuonekana kwa kila mwenye busara".

Ni miaka 32 imepita tangu maneno hayo yatamkwe. Nimeyanukuu kutokana na hali ilivyo hivi leo katika hii dunia yetu. Hivi sasa ni nani anaweza kunena kwamba dunia yetu isalama? Kila mwenye busara anaona dunia inawaka moto. Kila kitu kinaunguzwa. Dunia ile ambayo ilikuwa salama na amani haionekani. Dunia ile ambayo ilisheheni kheri na baraka tele haipo. Ramani yake kwa hakika inaonekana sehemu ndogo sana ya ardhi hii.

Kila janibu majanga ya kila namna yamejitokeza. Ardhi inaharibiwa kwa njia hii au ile. Watu maelfu kwa maelfu wanakufa. Hali ya salama na amani hivi leo ni ndogo mno. Zilikuwepo sehemu ambazo ziliaminiwa kuwa visiwa vya salama na amani na hizo Tanzania ikiwa m oja wapo. Nchi nyingi za Afrika, hasa za Kusini, walifanya Tanzania pahala pa kuishi kwa utuvu huku wakiendelea kudai uhuru wa nchi zao. Alhamdulillahi, kwa msaada wa Allah ndugu hao waliendelea kuishi nchini humu kwa usalama na amani hadi nchi zao zinakuwa huru.

Lakini Tanzania hali yake ya usalama na amani ikoje hivi sasa? Si swali gumu ni rahisi sana. Usalama na amani haupo tena kama pale zamani. Kuna sehemu ambayo wakazi wake wanaishi kwa wasiwasi sana. Nyumba za watu zinachomwa moto. Mashamba, magari na madaraja yanateketezwa na na mabarabara yanafumuliwa.

Inaya na kinaya imeingizwa katika fikira za watu. Unguja, Upemba na Ubara vimesimikwa katika mawazo ya baadhi yetu, mawazo ambayo yanakereketa kama nini sijuwi! Yanatishia hata muungano wa nchi zetu hizi mbili. Udini umepamba moto. Baadhi ya watu wameingiza udini hivi kwamba wanadadisi uwiano wa kila Sekta. Udini ni miongoni mwa mambo makubwa ninayoyaona yanachochea chuki badala ya upendo. Kitabu kitukufu cha Waislam cha Qur'an Tukufu kimebauliwa bila sababu yoyote chuki binafsi. Makanisa yamebomolewa na baadhi ya watu wamepoteza maisha yao.

Nishati ya gesi iliyopatikana kule Mikoa ya kusini na tukachekelea kupatikana kwa neema hiyo, n ayo pia imetuletea mtihani mkubwa. Kwa ajili yake hivi karibuni hapa, raia na baadhi ya maaskari wa



Mzee **Khamisi Wamwera**

jeshi la polisi wamepoteza maisha yao kwa kutupiana risasi na silaha za asili. Ni ajabu jambo la kuchinja nalo limeleta mvutano usioeleweka na kusababisha watu kadhaa kuumizwa na wengine kuuawa.

Nilifikiri viongozi wa siasa kwa busara zao na upevu wa kuelewa kwao mambo wangeweza kusaidia kuweka mambo sawa. Lakini cha ajabu na kushangaza sana ni kwamba wao wameongeza moto kwa kuweka petroli. Ndiyo hao walio mstari wa mbele kuwagawa wananchi kwa kanda. Ni hao wanaodai umuhimu wa ukabila na udini. Utofauti wa imani ya kisiasa umechochea chuki kati ya watu. Hata Wabunge wamechanganyikiwa. Wanazungumza mambo ya ajabu na ya khatari. Wanasema kuwa nchi watahakikisha haitawaliki. Haya ni machache miongoni mwa yale mengi ya hapa nyumbani. Hebu sasa nitoke nje.

Kuna nchi nyingi sana za Afrika nazo zimekumbwa na hali hii pia. Somalia ni nchi ambayo kwa miaka mingi sana haina usalama wala amani. Kwa muda mrefu imo kwenye vurugu na ghasia isiyokwisha. Wananchi wake wengi wameikimbia na kwenda kwenye nchi zingine kuwa wakimbizi. Bali nchi hii imetengeneza majangili wengi duniani. Ndiyo hao wanaovamia vyombo mbalimbali vitumiavyo bahari na kuteka waliomo humo na kupora kila kitu au kudai fidia kwa wenye chombo walichokiteka.

Wasomali wengi wameuawa. Sijui idadi yao sawasawa, lakini ni malaki ya watu kama si mamilioni. Watu hawa ni wa dini moja, wa n chi moja wenye koo tofauti wanamalizana. Punde hapa tumetangaziwa Serikali mpya ya Kiraia imechaguliwa, lakini bado hali ya nchi haijawa shwari na salama. Mkong'oto unaendelea na watu pamoja na nchi haijawa barabara.

Kongo mambo shaghalabaghala. Huko mambo ni magumu hasa. Huko wenyewe kwa wenyewe wanatifuwana. Zana mbalimbali za kivita zinapelekwa huko kwa kuuwa watu. Watu inasemekena mamilioni kwa mamilioni wameshapoteza uhai wao. Shaba na madini mengine yanasombwa na kupelekwa ughaibuni. Wananchi wanaachwa hoi bin taabani. Vizuri kuhadithiwa kama hivi, lakini walioonja vita hivyo cha moto wamekiona. Watu wanaacha watoto wao na wanakimbia bila kuelewa wanakoelekea. Vita ni khatari. Umoja wa Afrika umeshapeleka majeshi yake huko. Jeshi la wananchi wa Tanzania limepeleka maaskari wake. Lakini khabari zilizokuwa zimeenezwa kwenye vyomba vya habari ni kuwa askari wa Tanzania wamewahi kubaka huko, khabari ambazo zimekanushwa na jeshi la Tanzania.

Sudani mambo nako yamechacha. Wananchi wa Sudani ya Kaskazini na Kusini hawaivi pamoja. Upasi mkubwa umejitokeza kati yao. Mafuta yameleta ugomvi, bali vita ya wao kwa wao. Watu wanauwana.

Rwanda na Burundi nao hawapo salama. Jinamizi la vita limewakumba. Ubinafsi na ukabila umewaweka mahala pabaya sana. Kuna vita kali kati ya watusi na wahutu. Watu wanakimbia ardhi yao na kutelekeza mali zao. Watu wengi wamepoteza maisha yao na wengine wao wamekimbilia nchi jirani kuomba hifadhi.

Niger na Mali chokochoko imeanza na watu kadhaa wameshauwawa.

Endelea uk. 9

Je Bwana Yesu kwa mujibu wa Biblia ni Mungu au La?

Kutoka uk. 5

ya udhaifu iliendelea katika maisha ya Yesu, ndiyo sababu alijaribiwa na shetani, halafu alisulubiwa na Mayahudi. Katika 2 Wakorintho 13-4 tunasoma: Maana alisulubiwa katika udhaifu. Hapo watu wazushi wana tunga habari mpya kwamba Yesu Alisulubiwa kwa furaha yake na alibeba dhambi zetu. Jamani kama mtu anakubali kwa furaha yake, je inawezekana tena apige kelele na ahuzunike? Mathayo anasema, 26-39. Baba yangu, ikiwezekana, kikombe hiki kiniepuke. Alipokuwa msalabani alipiga kelele. Mathayo anasema 27-46; Yesu akapaza sauti kwa nguvu akisema, Eloi, Eloi lama sabakthani? Yaani Mungu wangu Mungu wangu, mbona umeniacha? Ndugu zangu Yesu alipiga kelele kwa sababu alijua kwamba kama atakufa msalabani hata kwa dakika basi atapata laana ya Mwenyezi Mungu, Kwa sababu alikuwa anajua maandiko ya (Kumb. 21-23); kwani aliyetundikwa amelaaniwa na Mungu. Jamani baadayakusomamaandikohaya siwezi kukubali kuunga mkono Mayahudi, ambao walijaribu kumuua Yesu msalabani ili alaaniwe na Mungu. Ndugu zangu tumfuate Yesu ambaye amesema, katika Yohana 17-3; Na uzima wa milele ndio huu, wakujue Wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma. (Kama mitume wingine, Yohana, David, Mussa n.k) Halafu Yesu alisema, katika Marko, 12-29, 31. Sikia Israel, Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja; nawe mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote, na kwa nguvu zako zote. Na ya pili ndiyo hii, mpende jirani yako kama nafsi yako. Hakuna amri nyingine iliyo kuu kuliko hizi. Ndugu zangu tumuabudu Mwenyezi Mungu mmoja sawa na amri kuu ya Yesu na tupendane au tusifuate hao wazushi. Kazi ni kwako.

Dunia - i - mazigazi, tunaelekea wapi hivi sasa?

Kutoka uk. 8

Naigeria mambo hayapo shwari hata kidogo. Boko Haramu wamejitokeza kupambana na Serikali. Hadi wakati huu, watu wengi wameuawa kwa silaha ya maangamizi.

Hata Asia haipo salama pia. Bangladeshi imekumbwa na majanga makubwa ya mafuriko. Kwa hilo, nchi hiyo imepoteza watu na mali nyingi. Inasemekana majumba kadhaa wa kadha yamesombwa na maji na mimeya ambayo ilikuwamo kondeni yote iling'olewa. Hakika msiba juu ya msiba.

Pakistani nayo hali yake ya usalama si nzuri. Pamoja na Serikali hiyo kuiwekea ngumu Jumuiyya ya Waislam Wa Ahmadiyya, lakini nayo inaonja adhabu kutoka kwa Allah. Ghadhabu ya Mwenyezi Mungu inawafikia nchini mwao bila wenyewe kutafakari. Mabalaa mbalimbali yamejitokeza na watu wameathirika kwa namna moja.

Nchi za Kiarabu ambazo zinajihesabu ni za Kiislamu, nazo zimekumbwa na hali mbaya ya usalama wa nchi zao. Huko amani haipo, bali kuna vita na ghasia. Badala ya watu kutawala, sasa bunduki zenye risasi, mabomu, vifaru na deraya mbalimbali za kivita, ndizo zinazoranda randa katika nchi hizo. Mchana watu wanajifungia ndani, usiku wanatafuta njia ya kutoroka nchini mwao.

Libya tangu atunguliwe Bwana Muammar Gaddafi, nchi haina utulivu. Neema ambayo waliitegemea wananchi wengi baada ya mapinduzi hayo sasa haionekani. Badala yake shida na matatizo mengi yanapandana. Watu wanauwana kila siku kwa mitutu ya bunduki na mabomu ya kujitowa mhanga.

Shia na Suni wanatwangana vibaya sana kule Iran na Iraq. Nchi hizo zimekuwa kaa la moto. Vita ipo kila siku ya Mungu. Watu wasiokuwa na hatia wanauawa kwa mabomu. Lebanoni, Siria na Kuweiti hali ni hii hii. Hakuna nafuu. Usalama na amani haionekani Giza la vita kila sehemu limezinga, watu hawaonani.

Misri haipo salama nayo. Imepondwapondwa na hadi sasa nchi hiyo hali yake ya usalama si ya kuridhisha. Mwanzoni walianzia maandamano tu, lakini waliponogezwa na fujo, wakaingia kwenye vita ya wenyewe kwa wenyewe. Waarabu wengi wamepoteza uhai wao. Tangu siku zile mpaka leo, nchi kiusalama haijawa sawa. Kila kiongozi anayechaguliwa au kuteuliwa na hawa, wale wa kule hawana imani naye. Mambo tafrani tupu.

Marekani, Amerika ya Kaskazini na kusini, Ulaya na Australia wapo powa. Wao wapo salama usalimini wala hawana uchafu huu wa kuvaana kwa vita. Kazi zao nikuwasha, kupulizia na kuchochea mataifa dhaifu yaingie vitani yenyewe kwa yenyewe kwa faida ya wakubwa haho. Wao ndiyo wanaouza silaha za vita zinazotumika hivi sasa sehemu mbalimbali za ulimwengu. Dunia inaelekea wapi hivi sasa?

Kuchanganya dini na siasa Kutatuchanganya

Kutoka uk. 10

wanasiasa cha kutoa zawadi za pesa kwa sura ya kuchangia harambee Makanisani na Misikitini kinaonekana machoni pa watu kama ni kiini macho kwa ajili ya kuteka akili za watu waonekane kuwa ni watu wema kumbe kinyume chake watu wamegundua kuwa hao wanasiasa wana ajenda ya siri ya kuutaka uongozi wa nchi hii. Kwa hiyo hivi sasa wakati tukielekea kwenye mbio za uongozi uchaguzi wa Rais na wabunge wa mwaka 2015 kumeibuka na baadhi ya wanasiasa wanaovuja mate kwa kuutamani uongozi huo.

Kwa mantiki hiyo tungewaomba wanasiasa wasichanganye dini na siasa kwani hiyo ni hatari wanaweza kuipeleka nchi yetu mahala pabaya. Wanasiasa wanatakiwa wafanye kama alivyofanya Bw. Yesu alipowajibu Mayahudi kuwaambia kuwa ya Kaisari mpeni Kaisari ya Mungu mpeni Mungu. Tarehe 08/05/2013 akifunga semina ya viongozi wa dini wa Mkoa wa Dar es salaam Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani Emanuel Nchimbi alitoa tamko la Serikali kuwa kutokana na hali ya wasiwasi na hofu kwa kuvunjika kwa amani kwa kuanzia sasa ni marufuku kwa mtu wa dini yoyote kutoa mahubiri ya kashfa dhidi ya dini nyingine.

Maelezo ya Mheshimiwa Waziri Nchimbi yanapaswa kuungwa mkono na kila mwana dini na mwananchi mpenda amani kwa Waislam Mwenyezi Mungu Ametueleza katika Qur'an Tukufu kuwa; "Uite watu kwenye njia ya Mola wako kwa hekima na mawaidha mema, na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora, hakika Mola wako ndiye Humjua sana aliyepotea katika n jia yake, naye Ndiye Awajuaye sana walioongoka" (16:126).

Tena Mwenyezi Mungu Anasema; " Wala msiwatukane wale ambao wanawaita kinyume cha Mwenyezi Mungu wasijewakamtukana Mwenyezi Mungu kupita kiasi bila kujua. Hivyo Tumewapambia kila watu vitendo vyao, kisha marejeo yao yatakuwa kwa Mola Wao, Naye Atawaambia waliyokuwa wakitenda" (6:109)

Aya hizo hapo juu zinawaeleza Waislamu kuwa wanapohubiri au kuzungumza na mtu yeyote kuhusu habari ya dini basi wajiepushe na maneno ya kashfa kama vile kudharau imani ya dini ya mtu mwingine au kutukana imani ya watu wengine, aidha neno "Bil Hikmat" lililopo katika sura ya 16:126 katika kamusi ya Akrab na Lane imesemwa maana yake uite watu kwenye njia ya Mola wako kwa kutumia Elimu au maarifa, uadilifu au haki, uvumilivu au upole, uwe imara, utowe mafunzo yaliyo kweli sawa na hali ya wakati, kipawa cha ufunuo na isiwepo tabia ya kijinga. Kwa mantiki hiyo ninawaasa Waislam wanapohubiri kwenye mihadhara yao waache kukashifu dini za watu wengine kwani kitendo hicho ni kumwasi Mwenyezi Mungu, bali kinachotakiwa kwenye mahubiri na mihadhara hiyo ni kuelezea ubvora wa mafundisho ya dini tukufu ya Kiislamu na mafundisho safi ya Mtukufu Mtume Muhammad (saw) kwani kinyume chake kama kutakuwa na mahubiri ya kashfa kuna uwezekano amani ikatoweka au wapinzani wa dini tukufu ya Kiislamu wanaweza kuitukana dini tukufu ya Kweli ya Kiislamu.

Pengine watu wanaweza kutatizwa kutokana na hali tete ya hofu na wasiwasi iliyopo hivi sasa hapa nchini petu. Pengine watu wangependa wapate majibu nini kifanyike ili amani ya kweli na ya kudumu iweze kupatikana hapa nchini petu, ningependa kutoa mwongozo kutoka kwa kiongozi Mtukufu wa Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya - Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as) ambaye pia ni Nabii wa Mwenyezi Mungu aliyetabiriwa kuja katika zama hizi za matatizo na maovu mengi, yeye alisema kwamba;

"Mwenyezi Mungu Amenituma ili kuanzisha uhusiano kati ya Mwenyezi Mungu na wanadamu ili haki za Allah (Mwenyezi Mungu) ziweze kutekelezwa. Pili nimetumwa kuanzisha upendo wa kweli miongoni mwa wanadamu wote, ili pia haki za Mungu ziweze kutekelezwa".
Kwa mantiki hiyo kama sifa hizi mbili zilizoelezwa na Nabii wa Mwenyezi Mungu Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as) zitatekelezwa basi nchi yetu ya Tanzania na nchi zingine duniani zinaweza kupata amani ya kweli na ya kudumu. Na siku hizi amani inahitajika kwa uhai wa dunia. Na amani inapatikana pale tu wanadamu watakapokubali kujenga uhusiano na Mwenyezi Mungu kwani tumeona na kusoma pia kwamba wale wanadamu waliokubali kujenga uhusiano na Mwenyezi Mungu kwa kuungana na Nabii wa Mwenyezi Mungu wamepata amani ya kudumu na ya kweli mfano halisi upo leo kwa wafuasi wa Jumuiyya ya Waislamu ya Ahmadiyya duniani kote wamekuwa watu wa amani na wanajisikia raha na utulivu katika mioyo yao kwa sababu tu wameungana na Mwenyezi Mungu kupitia kwa Nabii wa Mwenyezi Mungu Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as). Upendo na udugu ni muhimu sana kwa ajili ya maendeleo ya nchi yoyote duniani, bila upendo na udugu wa kweli amani ya kweli haiwezi kupatikana duniani na bila amani maendeleo hayawezi kufikiwa, na wale wanaopigana vita na kufanya vurugu duniani kwa jina la dini wanakosea sana pale wanaposema kuwa wanapigana kwa sababu ya kutaka uhusiano na Mwenyezi Mungu, kwa sababu Dini tukufu ya Kiislam inakataza kupigana au kufanya mauaji kwa ajili ya dini bali, bali Islam inafundisha na kuhimiza amani na maelewano katika jamii. Hivyo basi kujenga uhusiano na Mwenyezi Mungu ndio njia pekee ya kumaliza matatizo na mapigano yote ya vita Duniani.

Pia kiongozi Mkuu wa Jumuiyya ya Waislam ya Ahmadiyya Duniani hivi sasa Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (atbat) akitoa hotuba katika kongamano juu ya umuhimu wa amani Mjini London (March 2010) kiongozi huyo alisema kuwa; "Njia pekee ya kuleta amani duniani ni kumchagulia nduguyo kitu ambacho unajichagulia wewe mwenyewe".

Kiongozi huyo alliendelea kusema kuwa; "chimbuko la uhasama na kukosekana kwa amani duniani kunatokana na watu kujiona kwamba ni bora kuliko wengine, matabaka ya matajiri na masikini, kukosekana kwa fursa sawa kwa wote na kuingilia katika imani ya mtu".

Hivyo basi wasomaji wapendwa napenda kuiasa jamii kutafakari kwa makini maneno ya hapo juu ya viongozi wakuu wa Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya, naamini mwongozo mnaweza kuupata. Nami namwomba Mwenyezi Mungu Mtukufu Awaongozeni kwenye nuru ya kweli. Amin

= Mwisho=

Kuchanganya dini na siasa Kutatuchanganya

Kutoka uk. 12

makosa. Th.08/03/2013 waheshimiwa Maaskofu wapatao 177 walikusanyika katika ukumbi kituo cha mikutano na mafundinzo cha Baraza la Maaskofu katoliki Tanzania (T.E.C) Kurasini Jijini Dar es salaam, walikuwa wanajadiliana kuhusiana na hali tete iliyopo hivi sasa kutokana na mahusiano ya kidini kati ya Waislam na Wakristo. Kwa jumla katika mazungumzo yao waheshimiwa Maaskofu katika kikao chao waliilaumu sana Serikali kuwa ina udini inafumbia macho matatizo wanayoyapata Wakristo.

Pengine wasomaji wapendwa wangetaka kufahamu maana ya udini au ukabila maana yake ni nini udini au ukabila maana yake ni ubaguzi unaoendeshwa katika misingi ya kidini au ukabila, pia udini na ukabila una kawaida mbaya sana ya ubinafsi wa kubinafsishwa katika misingi ya kidini au kikabila, au kwa maana nyingine udini na ukabila ni kupendelea dini yako au kabila lako na kuwadhibiti watu wa dini au kabila lingine wasije wakapata mafao au mafanikio na maendeleo kama ya dini yako au kabila lako.

Na kwa upande wa baadhi ya Waislam nao wanailalamikia Serikali kwamba inawapendelea Wakristo wanatoa mfano wa mwaka 1992 ambapo inasemwa Serikali ilitiliana saini na Makanisa mkataba kwa siri, mkata ambao unalazimisha nchi yetu kutumia mabilioni ya walipa kodi wa dini zote kuhudumia shughuli za Kanisa. Aliyekuwa Makamu wa Rais na Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Alhaji Abood Jumbe Mwinyi katika kitabu chake kinachoitwa "The Partinership" (Muungano wa Tanganyika na Zanzibar miaka 30 ya dhoruba) ukurasa wa 125 Mheshimiwa Jumbe Mwinyi amesema kwamba ushahidi uliopo unaonesha kuwa Waislam wa Tanzania bara wamekuwa na uonevu wa kuendelezwa na kukoseshwa haki zao za msingi pamoja na katiba ya mwaka 1977 ilikuwa na vipengere vya kuhakikisha haki za binadmau na usawa kwa raia wote. Ushahidi wa ziada unaonesha kuwa kanisa nchini Tanzania ndilo linatoa maelekezo ya kisiasa, na mfumo wa kisiasa umekuwa ukifumwa kutoa upendeleo kwa Wakristo, ambao tayari wamo katika kudhibiti nafasi mbalimbali katika taasisi za umma. Alhajji Abuood Jumbe Mwinyi aliendelea kusema katika kitabu chake hicho katika ukurasa wa 132 - 136 ameandika takwimu mbalimbali za mashuleni (Sekondari) vyuoni na uteuzi wa viongozi serikali umefanyika upendeleo kwa Wakristo na Waislamu wamebaguliwa. Alhaji Jumbe ametoa mfano wa mwaka 1978 - 1981 wanafunzi wa Kiislamu walibaguliwa waliochaguliwa kwenda shule za Sekondari walikuwa ni 1978 Waislam asilimia 28, Wakristo asilimia 77, 1979 Waislam asilimia 22, Wakristo asilimia 78, mwaka 1980 Waislamu asilimia 23, Wakristo asilimia 77, mwaka 1981 Waislam asilimia 25, Wakristo asilimia 75. Wanafunzi wa kidato cha tano mwaka 1978 Waislam asilimia 12 Wakristo asilimia 88, a979 Waislam asilimia 13, Wakristo asilimia 87, 1980 Waislam asilimia 13 Wakristo asilimia 87, 1981 Waislam asilimia 12, Wakristo asilimia 88. Uteuzi wa viongozi wa Serikali mwaka 1993 Wakuu wa Mikoa walikuwa ni 20 kati yao Waislam walikuwa 5, na Wakuu wa Wilaya mwaka huo waliteuliwa 121 kati yao Waislam walikuwa 8, Makatibu wakuu wa Wizara mwaka huo waliteuliwa 20 kati yao Waislam walikuwa ni 4. Alhaji Jumbe anaeleza katika kitabu chake ukurasa wa 138 kwamba picha inayooneshwa na taarifa za takwimu hizo ni kuwa Waislamu pamoja na kuonyeshwa kuwa kuna vifungu vya katiba vyenye kulinda haki hizo basi bado wao wananyimwa haki za usawa na za kutosha".

Hayo hapo juu ndiyo malalamiko kwa upande wa Waislam na Wakristo dhidi ya Serikali. Na kwa upande wa Wanasiasa nao pia wanayo malalamiko yao kwa mfano gazeti la kila siku la Mtanzania la tarehe 16/04/2013 amenukuliwa Mheshimiwa Mbunge wa Rombo Joseph Selasini (CHADEMA) wakati akiwa bungeni akichangia hotuba ya bajeti katika Ofisi ya Waziri Mkuu alinukuliwa na vyombo vya habari akisema kwamba "Naiambia Serikali hakuna haja ya (kuitisha) kikao cha viongozi wa dini kwa sababu suala hili la udini, limepandikizwa na linasimamiwa na baadhi ya viongozi ndani ya Serikali, nasema hivi kwa sababu mengi yanayofanyika katika nchi hii kuhusu udini, ni uvunjifu wa sheria na ninashangaa kwa nini hatua hazichukuliwi kwa hao wanao vunja sheria".

Mheshimiwa Mbunge Joseph Selasini aliendelea kusema; "Kwa mfano hiki chuo cha (UDOM) Dodoma kinachomilikiwa na Serikali ambacho kwa sasa kinaendeshwa kama chuo cha kidini (cha Kiislamu) ninayo kanda (CD) inayoonyesha hayo. Wanafunzi fulani (yaani Waislamu) pamoja na Wahadhiri wa dini fulani (Waislam) ndani ya (UDOM), walikusanywa wakapewa siasa za chuki dhidi ya (wanafunzi) wenzao wa dini fulani (Wakristo)"

Kwa jumla maneno



Mwl. Kais Ali

aliyoyaongea Mheshimiwa Mbunge wa Rombo Joseph Selasini (CHADEMA) alikuwa anailaumu Serikali kwa kuzembea kwa kutosimamia sheria kwa kuendelea kuwaacha watu wanavunja sheria za nchi kwa kuwaacha watu wanaeneza udini hata katika taasisi kubwa za kitaifa kama chuo kikuu cha UDOM. Ingawa maelezo ya Mheshimiwa Mbunge Joseph Selasini yalijibiwa vizuri sana na Waheshimiwa Mawaziri kwa mfano Waziri wa nchi katika Ofisi ya Rais (Utumishi) Mheshimiwa Stephen Wassira tarehe 18/04/2013 wakati akiwakilisha hotuba ya Bajeti yake alipinga maelezo ya Mbunge wa Rombo yaliyotolewa Bungeni na baadhi ya wabunge waliosema kwamba Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Kikwete kuwa ina udini. Mheshimiwa Waziri Wassira alitoa mfano kuwa katika Ofisi ya Rais (yaani Ikulu) ukimwacha yeye mwenyewe Mheshimiwa Rais ambaye ni Mwislam lakini watumishi wote wanaobakia ni Wakristo watupu, kwa kigezo hicho Mheshimiwa Waziri Wassira alihoji kwamba hapo udini upo wapi kwa Rais Kikwete? Waziri Wassira aliendelea kusema kuwa Suala la udini lina kuzwa zaidi na watu wenye malengo mabaya ya kisiasa, tangu huko nyuma hata Zanzibar yenye Waislam aslimia 90 hawajawahi kuitangaza Zanzibar kuwa ni nchi ya Kiislam. Waziri Wassira aliendelea na na maelezo yake kuwa udini ulichochewa na wanasiasa uchaguzi wa mwaka 2010 kwa sababu ya watu kutaka madaraka, mwaka huo haukua mzuri sana (Kisiasa), lakini tuyaache yaliyopita si ndwele. Wahenga walisema; "Usipoziba ufa utajenga ukuta". Waziri Wassira katika maelezo yake alimnukuu Baba wa Taifa Mwalimu J.K. Nyerere akisema kuwa ; "Ukisikia wanaopaza sauti zaidi sauti za udini ndio (wao) wanaoeneza", kwa hiyo tuwe makini na wanaopiga kelele juu ya jambo hilo (la udini). Waziri Wassira aliendelea kusema kwamba ni vema Bunge litafute namna bora ya kushughulikia suala hili ili lisiendelee kuwa kikwazo kwa amani ya nchi yetu".

Pia ifahamike kuwa baadhi ya viongozi wakuu waandamizi katika chuo kikuu cha UDOM ni Waislam kwa mfano Prof. Idrisa Kikula ni Makamo (Vice Chancellar) na Dr. M. G. Bilal ni (Chairman of Council) hivyo basi Mheshimiwa Mbunge wa Rombo Joseph Selasini (CHADEMA) alipoona Mheshimiwa Rais Kikwete ambaye ni Mwislamu kwa dini yake, amewateua Bw. Prof. Idrisa Kikula na Dr. M. G. Bilal ambao pia ni Waislamu kuwa viongozi wa pale chuoni (UDOM) yeye Mheshimiwa Mbunge Selasini akadhani kuwa Rais Kikwete amefanya uteuzi huo kwa upendeleo kwa sababu ya udini, kumbe angeangalia orodha ya majina ya viongozi wakuu wa pale chuoni (UDOM) angegundua kuwa viongozi wengi pale chuoni (UDOM) ni Wakristo kwa mfano Mkuu wa chuo (Chancellar) ni H.E. Benjamin William Mkapa (Mkatoliki), Principal College of Education ni Prof. K.M. Osaki ni (Mkatoliki), Principal College of Humanities ni Prof. C.M Rubagumya (Mkristo), Principal College of Information ni Prof.N.Mvungi (Mkristo Protestant). Kwa mantiki hiyo orodha ya viongozi wa UDOM hapo juu inaonesha Wakristo ni wengi kuliko Waislam. Hivi sasa Taifa limepatwa na hofu kubwa sana na viongozi wa Serikali wamekuwa na wasiwasi kutokana na mambo ya kigaidi na mabaya yanayojitokeza hivi sasa hapa nchini petu ni mambo ya kikatili ambayo hayajawahi kutokea miaka ya nyuma iliyopita.

Tarehe 05/05/2013 kwa masikitiko makubwa sana Kanisa la Mtakatifu Joseph Mfanyakazi Parokia ya Olasiti Mkoani Arusha kulipigwa na bomu kuliko pelekea watu 3 kupoteza maisha na watu 60 kujeruhiwa tunamuomba Mwenyezi Mungu Awasamehe Makosa yao marehemu hao na Awape afya mzuri majeruhi waliopatwa na mkasa huo wa kifedhuli, sawa na taarifa kutoka katika vyombo vya usalama anayetuhumiwa kufanya kitendo hicho cha kinyama kwa mujibu wa maelezo ya kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha Liberatus Sabasi alimtaja Bw. Victor Ambrosendiye anayetuhumiwa kutupa bomnu hilo na tayari amekwishafikishwa mahakamani kwa ajili ya kujibu mashtaka hayo. Pamoja na mambo mengine yaliyojitokeza hivi karibuni Mwezi Februari ya kuuawa kwa Padre Evarist Mushi wa Kanisa la Katoliki visiwani Zanzibar mambo hayo yote kwa ndugu zetu Wakristo wanayaona kuwa ni kwa sababu ya udini. Mambo hayo ni ya kinyama ambapo yanapaswa kulaaniwa na kila mwanadini na mpenda amani kwa sababu hakuna dini yeyote yenye kuamirisha kufanya matendo mabaya na ya kinyama kama hayo. Ingawa mlipuaji wa bomu hilo Bw. Victor Ambrose siku ya tukio inasemwa kuwa alivalia nguo ya kanzu inayovaliwa na Waislamu ili ionekane kuwa aliyefanya kitendo kile ni Mwislama lakini alipokamatwa na waumini pale kanisani siku ile ya tukio iligundulika kuwa yeye ni Mkristo na ni mkazi wa Rombo Mkoani Arusha. Tunawashukuru viongozi mbalimbali wa Serikali na wa vyama vya siasa wamelaani kitendo hicho cha kinjama.

Mheshimiwa Waziri Mkuu Perter Pinda tarehe 06/05/2013 alikwenda Mkoani Arusha kuwapa pole majeruhi walioathirika na mkasa huo wa kulipuliwa kwa bomu pia aliwapa pole wafiwa walio ondokewa na ndugu zao, akiwa huko Mkoani Arusha Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema kuwa matendo yanayofanyika hapa nchini petu hivi sasa ya kuwauwa viongozi wa dini au waumini hayakubaliki na wala mtu asifikirie kuwa kumwua Padre, Mchungaji au Sheikh ndio utakuwa umeiuwa dini ya Kikristo au ya Kiislamu huko ni kujidanganya bali Ukristo na Uislamu utaendelea kusonga mbele.

Pia Mheshimiwa Mbunge Habibu Mnyaa (CUF) wa Mji Mkongwe Zanzibar akichangia bungeni Dodoma baada ya kuletwa taarifa ile ya mlipuko wa bomu pale bungeni alisema kwamba nchi hii ya Tanzania ni nchi ya watu wote Wakristo na Waislamu na wala mtu yeyote asifikirie kuwa ataitawala nchi hii kwa kupitia mgongo wa dini fulani huko ni kujidanganya.

Hivi sasa wanasiasa nao wanalaumika kwa tabia ya kuchanganya dini na siasa, wapo wanasiasa hivi leo wanajitafutia umaarufu kwa kupitia mgongo wa dini baadhi ya wanasiasa wameonekana wakijipenyeza hata katika majumba ya ibada, Makanisani na Misikitini wanagawa zawadi za pesa na pia kuna baadhi ya viongozi wa dini ambao hivi sasa wanaonekana na jamii kuwakumbatia wanasiasa hao baadhi ya viongozi wa dini wanaonekana kuthubutu kuwatunuku tuzo ya amani baadhi ya wanasiasa. Kwa mfano gazeti la kila wiki la Mwanahabari la Jumatatu April, 8 - 14 mwaka huu wa 2013 uk. 2 mwandishi wa gazeti hilo amenukuliwa akifanya mahojiano na Sheikh wa Mkoa wa Dar es salaam akimhoji kwa nini Sheikh ametoa tuzo ya amani kwa mwana siasa fulani ambaye pia aliwahi kuwa Waziri Mkuu lakini alijiuzulu kwa hiyari yake. Pengine kitendo hiki kinachofanywa na

Endelea uk. 9

Ujumbe wa amani kwa Tanzania

Kutoka uk. 12

makusudio ya siri ya Mwenyezi Mungu Aliyechukizwa, yaliyokuwa yamefichika hadi sasa, yamedhihirika. Mungu Anasema; Huwa Hatuadhibu hadi Tumletapo Mtume. Wale wenye kutubu wataukuta usalama na wale watakaoogopa (Mungu) kabla ya kukutwa na majanga wataonewa huruma.

Mnadhani mtayaepuka majanga haya? Je mnaweza kujiokoa kwa kupitia ustadi au mbinu? Hata kidogo. Siku hiyo mipango yote ya kibinadamu itashindwa. Msidhani kwamba matetemeko ya ardhi yalifika tu Amerika na kwenye mabara mengine na kwamba nchi yenu itabakia salama. Kwa hakika mnaweza kupata shida zaidi. Ewe Ulaya! Hauko salama na ewe Asia, wewe pia haujaepukana. Na enyi wakazi wa visiwani, Hakuna miungu ya bandia itakayokuja kukuokoeni. Naiona miji ikianguka na makazi yakiharibiwa. Mungu Mmoja na wa Pekee Alikaa kimya kwa muda mrefu. Matendo maovu sana yalitendwa mbele ya macho yake na Hakusema chochote. Lakini sasa Ataudhihirisha uso wake kwa ujalali na haiba. Mwenye masikio na asikie kwamba wakati huo haupo mbali. Nimejitahidi kwa kadiri ya uwezo wangu kuwaleteni nyote chini ya hifadhi ya Mwenyezi Mungu, lakini ilikadiriwa kwamba kile kilichoandikwa ni lazima kitimie. Ninasema kwa ukweli kwamba zamu ya nchi hii pia yakaribia kwa kasi. Zama za Nuhu zitatokea tena mbele ya macho yenu na macho yenu wenyewe yatashuhudia majanga yaliyoikumba miji ya Lut. Lakini Mwenyezi Mungu si Mwenye haraka katika ghadhabu Zake. Tubuni ili muonewe huruma! Yule asiyemuogopa ni mfu, si hai." (Haqiiqatul Wahyi uk 256 – 257).

KHALIFATUL Masih wa tatu wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya, Hadhrat Mirza Nasir Ahmad rh.a. aliitahadharisha dunia kwa kusema:

"Lakini Enyi waungwana! Tusisahau kwamba bishara hii, kama zilivyo bishara zingine zote, ni onyo ambalo kutimia kwake kwaweza kuahirishwa au hata kuzuiwa kabisa kama mwanadamu atarejea kwa Mola Wake, akitubu madhambi yake na kuirekebisha mienendo yake. Bado anaweza kuizuia hasira ya kimbingu kama ataacha kuiabudu miungu bandia ya utajiri, mamlaka na ufahari, kama atastawisha uhusiano wa uaminifu na Mola Wake, kama atajiepusha na udhalimu wote, kama atayatekeleza majukumu yake kwa Mwenyezi Mungu na kwa mwanadamu na kujifunza kutenda kwa ajili ya ustawi wa kweli wa wanadamu.

"Yote haya yanategemea mataifa yale yanayoitawala dunia leo, ambayo yamelevywa na kinywaji kikali cha utajiri, mamlaka na ufahari, je wako tayari kuondokana na hali hii ya kulevywa? Je wako tayari kupokea neema na furaha hii ya kiroho? Kama sivyo, basi ghadhabu za kimbingu ni lazima zitateremka. Kama hawaachani na mienendo yao miovu na kung'ang'ania kwenye kiburi, basi hakuna nguvu wala miungu hiyo ya bandia iwezayo kuwaokoa na adhabu hiyo iliyoahidiwa. Hivyo jihurumieni wenyewe na watoto wenu, isikilizeni sauti ya Mola wenu Aliye Mwingi wa Rehema na Mwingi wa Ukarimu. Awajaalieni tabasamu lake la upendo na Awapeni nguvu ya kukubali na kunufaika na ukweli."

Hivyo wapenzi waheshimiwa, mabibi kwa mabwana, salama yetu sote imo katika kuambatana na Jumuiya hii ya Waislamu wa Ahmadiyya, Jumuiya iliyoanzishwa na Mwenyezi Mungu kueneza suluhu na maelewano, dhehebu hili halina uhusiano wowote ule na vita na mapigano. Dhehebu hili linatoa habari njema kwa kila anayetaka amani na suluhu. Tangu azali, ndani ya vitabu vya manabii, ilishatolewa habari ya dhehebu hili lenye baraka, na kuna ishara nyingi sana za kudhihiri kwake. Nini tena kiandikwe zaidi, Mwenyezi Mungu Atie baraka ndani ya jina hili, Mwenyezi Mungu Ajaalie kwamba Binadamu wote duniani waingie ndani ya dhehebu hili ili sumu ya umwagaji damu wa binadamu itoke kabisa mioyoni mwao, na wawe wa Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu Awe wao. Ewe Mkarimu na Mwenye Uwezo! ufanye hivyo, Amin"

Hivyo enyi ndugu zangu, sikilizeni kwa makini: Nuru ile iliyoangaza juu ya mlima Sinai, nuru ile iliyoyamulika maisha ya wavuvi wa Galilea, nuru ile iliyoiangaza dunia toka kwenye vilele vya mlima Faran, nuru hiyo hiyo leo imetumulika tena toka kwenye sehemu isiyo maarufu ya Qadian, kando ya mto Beas. Mwenyezi Mungu Atastawisha ukweli, haki, upendo na amani duniani kupitia Ahmad a.s., mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya, aliyedhihiri katika kijiji cha Qadian, India, zaidi ya miaka mia moja iliyopita. Mahusiano ya kudumu kati ya Mwenyezi Mungu na wanadamu yataimarika, waovu wataacha dhulma zao na wema utatapakaa duniani. Wamebarikiwa wale wafanyao amani na Mwenyezi Mungu. Ahsanteni.

HATI YA MTUME S.A.W. KWA AJILI YA WAKRISTO

"Hii ni hati ambayo Muhammad bin Abdullah, mtume wa Mungu, Mwonyaji na Mletaji wa Habari Njema, ameiandikisha ili pasibakie udhuru wowote kwa hao watakaokuja baadae. Nimeiandikisha hati kwa ajili ya Wakristo wa Mashariki na Magharibi, kwa ajili ya wale wanaoishi karibu na wale wanaoishi katika nchi za mbali, kwa wakristo walio hai sasa na wale watakaokuja baadae, kwa ajili ya Wakristo tunaowajua na wale tusiowajua.

"Mwislamu yeyote atakayevunja na kuyapuuza yaliyoamrishwa ndani yake, atafahamiwa kuwa ni mvunjaji wa agano la Mungu na atakuwa ni mvunjaji wa ahadi Yake na atajifanya mwenye kustahili laana ya Mungu, awe Mfalme au Raia.

"Ninaahidi kuwa mmonaki yeyote au mpita njia n.k. atakayetaka msaada wangu juu ya milima, ndani ya misitu, majangwani, au kwenye maeneo wanayoishi watu na katika sehemu za ibada, nitawafukuza maadui zake na kumlinda, nikishirikiana na rafiki zangu wote, na wasaidizi wangu, pamoja na jamaa zangu wote, pamwe na hao wanaodai kunifuata, kwa sababu wao ni raia wangu nami ninawapa kinga, yaani wako juu ya agano langu. Nami nitawalinda waliopewa agano wasiteswe, wasijeruhiwe na wasisumbuliwe na maadui zao. Na kutokana na hayo, watalipa kodi ya Jizya ambayo wameahidi kuitoa.

"Wakipendelea wenyewe kuzilinda mali zao na nafsi zao, wataruhusiwa kufanya hivyo na hawatapewa ugumu wowote katika jambo hilo. Hakuna askofu atakayefuzwa katika mamlaka yake, wala Mmonaki katika Monaki yake, na wala Kasisi katika eneo lake la ibada, na hakuna mwenye kuhiji atakayezuiwa katika Hija yake.

"Makanisa yao na sehemu zao zingine za ibada hazitanyang'anywa au kuteketezwa au kuvunjwa, vifaa vya Makanisa yao havitatumiwa kujengea Misikiti au nyumba za Waislamu. Mwislamu yeyote atakayefanya hivyo afahamike kuwa amemwasi Mungu na Mtume Wake. Mamonaki na Maaskofu hawatatozwa kodi ya Jizya au ya kujikomboa, wawe waishio misituni au mitoni, Mashariki au Magharibi, Kaskazini au Kusini. Ninawapa ahadi yangu. Wako juu ya ahadi yangu na agano langu na watakaa kwa salama kabisa wasipate kila namna ya udhia.

"wanaoishi milimani na kwenye sehemu zao za Wakfu, mazao ya mashamba yao hayatatozwa kodi, na katika nyakati za upungufu wa chakula, hawatalazimishwa kutoa mchango wowote wa nafaka. Hawatafanyishwa kazi za vita wala hawatatozwa kodi ya Jizya. Wafanya biashara wao, wamiliki wao wa ardhi na matajiri wao watatozwa Dirham zisizozidi kumi na mbili kwa mwaka. Wasisumbuliwe na kufanyiwa jeuri katika ulipaji wa kodi. Katika mijadala na midahalo wazungumzwe nao kwa adabu na upole.

"Basi Rehema iwafunikize popote walipo na walindwe na kila namna ya taabu na udhia. Avunjae agano la Mungu na kufanya ushindani, atafahamiwa kuwa ni adui wa Mungu na mvunjaji wa agano Lake. Wapewe kila namna ya msaada katika kutengeneza Makanisa yao yanapoharibika. Watapewa uhuru wa kutochukua silaha. Watalindwa na Waislamu. Basi, hati hii isikose kutiiwa mpaka siku ya Kiama." (Futuuhul Buldaan Balazaar).

BRAZIL BINGWA!

Na Ayoub Mtekateka,
Dar es Salaam

Magoli mawili yaliyofungwa na Fred na moja kutoka kwa Neymar yalitosha kabisa kuipa Brazil ubingwa wa Kombe la Mabara kwa mara ya nne wakiitandika Hispania magoli 3-0 katika mchezo wa fainali ya kombe la mabara uliochezwa mwishoni mwa wiki iliyopita katika uwanja wa Estadio Jornista Mario Filnho maarufu kwa jina la Maracana uliopo katikati ya jiji la Rio De Jeiro nchini Brazil.

Brazil ambao ni maarufu kama 'Les Selecao' ilikuwa ni mwenyeji wa mashindano hayo ambayo hufanyika mwaka mmoja kabla ya kuanza kwa michuano ya kombe la Dunia, ilikuwa na kila sababu ya kushinda mechi hiyo iliyohudhuriwa na mashabiki wapatao elfu nane waliokuwa na hamu kubwa ya kuiona nchi yao ikinyakuwa mwali mbele ya macho yao tena katika ardhi yao ambayo mpira unaabudiwa zaidi kuliko kitu chochote kingine.

Wachezaji wa Brazil wakishangilia goli la tatu lililofungwa na Fred (aliyenyoosha mkono) dhidi ya Hispania katika mchezo wa fainali ya Kombe la Mabara uliochezwa kwenye uwanja wa Estadio Jornista Mario Filnho 'Maracana', Rio Di Jeneiro, Brazil. Katika mchezo huo, Brazil ilishinda 3-0 na kunyakua Kombe hilo. (Picha na Ayoub Mtekateka kwa msaada wa Mtandao)

Wenyeji walikuwa katika kiwango cha juu katika mchezo huo huku wakiwa na rekodi nzuri ya kushinda michezo 29 ya kimataifa bila kufungwa wakiandika historia ya kipekee kwa kuwafunga Hispania maarufu kama 'la Roja', mabingwa wa bara la Ulaya na Dunia katika ardhi yao. Brazil pia iliwahi kulinyakua kombe hilo mwaka 2009, 2005 na 1997.

Ilimchukua sekunde 90 tu



Wachezaji wakishangilia baada ya ushindi

kufungua ukurasa wa mabao kwa timu ya Brazil, kabala ya mshambuliaji mpya wa Barcelona, Neymar kufunga goli la pili dakika chache kabla ya mapumziko.

Brazil waliendelea kulisakama lango la Hispania mwanzoni mwa kipindi cha pili wakati Fred alipoubabatiza katikati ya mabeki wa Hispania na kliteta kizazaa kilchosababisha Sergio Ramos kuunawa mpira huo lakini mwamuzi hakuiona penati ya wazi.

Kadi nyekundu aliyopewa Gerard Pique kunako dakika ya 68 ilitosha kabisa kuzima matumaini ya 'la Roja' kuweza kusawazisha magoli hayo licha ya kupewa nafasi kubwa ya kunyakua taji hilo kwa mara ya pili mfululizo na kujikuta ikiachia mwanya kwa Fred kupigilia msumari wa mwisho kwa Brazil akifunga bao safi lililoamsha kelele za mashabiki waliokuwa wakishangiliwa kwa fujo . Ushindi huo wa Brazil, umetibua rekodi ya Hispania ambayo haikuwahi kufungwa magoli kama hayo katika mashindano ya kimataifa tangu mwaka 1985.

Golila Fred ambaye anaichezea klabu ya Fluminence ya Brazil lilitokana na kazi nzuri iliyofanywa na Oscar aliyetoa krosi safi na kumkuta mfungaji akiwa kaika nafasi nzuri ya kufunga katikati ya mabeki wa Hispania Alvaro Arbeloa na Gerrard Pique na kumwacha golikipa Ike Cassilas akiutazama mpira ukiingia golini kwake.

Hispania walipata nafasi kadhaa kuweza kusawazisha lakini juhudi za washambuliaji wake Pedro na David Villa ziliishia mikononi mwa mlinda mlango wa Brazil, Cesar aliyekuwa makini kuzuia mashuti yao kwa umakini dakika chache kabla ya kipyenga cha mwisho.

Lakini haukuwa usiku wa 'la Roja' kama ilivyotarajiwa na mashabiki wengi wa soka ulimwenguni wakati mwamuzi B Kuiper akipuliza filimbi kuashiria kumalizika kwa mechi hiyo kali.

Swali kubwa linaibuka hapa kama Brazil wataendeleza ubabe wao hadi wakati wa michuano ya kombe la Dunia mwaka 2014 au vinginevyo? Tusubiri tuone panapo majaaliwa. Tuonane wakati mwingine, In Sha Allah.

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

MapenziyaMungu

Sha'baan 1434 AH | Juni 2013 | Ihsan 1392 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Huraira r.a. ya kwamba Mtume s.a.w. alisema: Hakika Mwenyezi Mungu Haiangalii miili yenu wala sura zenu bali Huziangalia nyoyo zenu (kwamba mle ndani mna Ikhlasi kiasi gani). (*Muslim*)

Khalifa Mtukufu: Serikali ziwatendee wema raia wake

Na Mwandishi wetu, Dar es Salaam

Kiongozi wa Jumuiya ya Waislam Ahmadiyya Duniani, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a, Khalifa wa tano wa Masihi Aliyeahidiwa (a.s), ameelezea umuhimu wa dua na maombi kutokana na hali ya hatari na machafuko ya dunia iliyopo hivi sasa.

Kiongozi huyo wa Waislam pia alizitaka Serikali zote kuwatendea raia wake kwa huruma, haki na usawa.

Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.ba, Kiongozi wa Jumuiya ya Waislam Ahmadiyya Duniani

Akitoa hotuba ya Ijumaa kwenye Msikiti wa Baitul Futuh huko Kusini Magharibi mwa jiji la London, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a alisema kuwa ni muhimu kwamba Waislam Waahmadiyya waombe kupata "Hasana", ambalo ni neno la Kiarabu lenye kumaanisha kila aina ya wema na baraka.

Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a amesema:

"Katika baadhi ya nchi, wapinzani wa Jumuiya yetu hutaka Waislam Waahmadiyya waondolewe kila aina ya baraka za Mwenyezi Mungu. Hivyo, tunatakiwa tuwaombee majirani zetu wasitusababishie huzuni na mateso yoyote, na tuiombee miji yetu na nchi zetu kuwa chanzo cha furaha yetu na kutosheka kwetu."

Aidha, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a aliendelea kuzungumzia hali ya utawala wa baadhi ya nchi za Kiislam:

"Katika baadhi ya nchi za Kiislam tunaona kwamba watawala au serikali ndio wamekuwa chanzo cha mateso na kupoteza matumaini kwa watu wao. Hivyo, tunatakiwa tuwaombee viongozi wa nchi zote waweze kuwatendea watu kwa haki, kuwahurumia na kuwafanyia uadilifu. Kama hawawezi kujirekebisha, basi tuombe kwamba wapatikane viongozi na serikali nyingine ambazo zitazingatia sifa hizi njema."

Kiongozi huyo wa dunia alitoa shukrani zake kwa watu ambao si wanajumuiya Ahmadiyya lakini wamekuwa wakiwahurumia na kuwasaidia Waahmadiyya bila kujali tofauti za kiimani.

Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a amesema:

"Nchini Pakistan na katika baadhi ya nchi, huku kukiwa na wale ambao wamekuwa wakishawishiwa na viongozi wa dini wenye msimamo mkali na hivyo kujaribu kuwadhuru Waislam Ahmadiyya, pia lipo kundi la watu ambao wameonyesha kuwa wema na marafiki waaminifu kwetu. Kwa kweli wanatuhurumia, wanatutakia mema na kutusaidia katika nyakati za tabu na mtihani."

Mwisho



Kiongozi wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya Duniani, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a

Ujumbe wa amani kwa Tanzania

Hotuba iliyotolewa na Sheikh Bakri Kaluta katika mkutano wa amani - Morogoro 2013

Kutoka toleo lililopita.

Vita ya tatu ya dunia n-ayo ilitabiriwa na Mwanzilishi Mtukufu wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s., kwamba kambi hizo mbili zenye kuhasimiana zitajikuta zimeingia katika mapigano ya ghafla yasiyotegemewa, ambapo vifo na maangamio vitashuka toka mawinguni na mioto mikali itaikumba dunia, sanamu la ustaarabu wa siku hizi litaporomoka, pande zote mbili zitaangamia, watakaosalimika watapigwa butwaa kutokana na maangamio yaliyojiri. Warusi walitabiriwa kupata ahueni mapema kutoka katika janga hilo, na kwamba wengi wao wataipokea haki na kuwa Waislamu wa Ahmadiyya. Haya ni maneno ya Mwenyezi Mungu, alisema, ni lazima yatatimia tu.

Hadhrat Ahmad a.s. alisema:

"Kumbukeni! Mwenyezi Mungu Amenifahamisha kuhusiana na matetemeko mengi ya ardhi, kwa hiyo



Sheikh Bakri Abedi Kaluta

kuweni na uhakika kwamba, kama vile matetemeko ya ardhi yalivyoitikisa Amerika na Ulaya, vivyo hivyo yataitikisa Asia. Baadhi yao yatafanana na siku ya Kiama. Watu wengi sana watakufa kiasi ya kwamba mito ya damu itatiririka. Hata ndege na wanyama wakali hawatasalimika na kifo hiki. Maangamio makubwa yataifagia sura ya ardhi ambayo yatakuwa ni makubwa kuliko yote tangu kuumbwa kwa mwanadamu. Makazi yatateketezwa kana kwamba hakuwahi kuishi humo yeyote. Hii itafuatiwa na majanga mengine mengi yaliyo mabaya yatakayoletwa na ardhi na mbingu hadi hali yake isiyokuwa ya kawaida itakapodhihirika wazi kwa kila mwenye busara. Maandiko yote ya sayansi na falsafa yatashindwa kuonyesha mfano wake, ndipo mwanadamu atakapochanganyikiwa kupita kiasi na kupigwa butwaa kwamba sasa nini kitatokea. Wengi watasalimika na wengi wataangamia.

"Siku hizo zinakaribia kwa hakika, bali naweza kuziona ziko mbele yangu, wakati dunia itakaposhuhudia maono ya kutisha: sio matetemeko tu ya ardhi, bali majanga mengi ya kutisha yatamkumba mwanadamu, mengine yakitokea mawinguni na mengine ardhini. Haya yatatokea kwa sababu wanadamu wameacha kumuabudu Mungu wao wa kweli na kujitokomeza katika masuala ya kidunia kwa mioyo yao yote na juhudi na dhamira zote. Kama nisingekuja, pengine majanga haya yangeahirishwa kidogo, lakini kwa kuja kwangu,

Endelea uk. 11

Kuchanganya dini na Siasa Kutatuchanganya

Na Mwl. Kaisi Ali wa Mkongotema Madaba Songea

Mwaka 1995 ulipoanza uchaguzi wa mfumo wa vyama vingi kabla ya uchaguzi kufanyika Baba wa Taifa Hayati Mwalimu J. K. Nyerere alitoa hotuba akizungumzia suala udini alisema kwamba, "Hivi sasa hapa nchini petu kuna baadhi ya watu wangetaka nchi hii ya Tanzania iwe nchi ya kidini ya Kikristo au ya Kiislamu. Aliendelea kusema kwamba watu wazima wenye akili timamu hawawezi kamwe kuzungumzia udini hapa nchini petu kwa sababu nchi yetu siyo ya kidini". Mwalimu Nyerere alichukizwa sana na jambo hilo la kuzungumzia udini na ukabila akafika mbali zaidi hata akathubutu kutamka kwamba kuzungumzia udini na ukabila huo ni upumbavu na ni hatari.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo ni sheria mama katika ibara ya 3 - (1) inatamka wazi kuwa, "Jamhuri ya Muungano ni nchi ya Kidemokrasia na ya kijamaa, isiyo kuwa na Dini yenye kufuata mfumo wa vyama vingi vya siasa". Kwa mantiki hiyo nchi hii ya Tanzania sio nchi ya dini fulani bali ni nchi ya watu wa dini zote na hata yule asiye kuwa na dini pia ana haki ya kujiita Mtanzania na wala wafuasi wa dini fulani hawana hati miliki ya nchi hii Wakristo, Waislam na Wapagani wote ni nchi yetu. Kwa kuwa wote tumezaliwa humu. Hivi sasa imepita miaka 18 tangu baba wa Taifa azungumzie na kukemea suala la udini na ukabila. Hivi karibuni kumeibuka tabia mbovu kwa baadhi ya jamii za Watanzania kuzungumzia habari ya udini na ukabila ingawa jambo hilo halikuwapo wakati wa Mwalimu Nyerere. Hivi sasa imebainika kuwa baadhi ya Waislamu na Wakristo wanailalamikia Serikali hasa hasa ndugu zetu Wakristo wanaosema kwamba Serikali haijali matatizo yao wanayofanyiwa kwa mfano kuchomwa kwa Makanisa yao zaidi ya (30) na kuuawa kwa viongozi wao wa Kanisa na Waislamu, bado Serikali imenyamaza kimya bila kuwashughulikia wahusika ambao ni Waislamu, kitendo hicho ndugu zetu Wakristo wanasema kwamba Serikali inayoongozwa na Mh. Rais J.M. Kikwete ambaye kwa dini ni Muislam ana udini kwa sababu anawapendelea Waislam wenzake kwa kutowachukulia hatua Waislam wanapofanya

Endelea uk.10